# USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA ZA *NATALA NA MAMA EE*

NA

ONYONI JOYCE KWAMBOKA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library
0389741 0

NOVEMBER 2012

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katik chuo kingine chochote.

Saini________________ Tarehe 2/11/2012

Onyoni Joyce Kwamboka

Kazi imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi tulioteuliwa na Chuo Kikuu ch Nairobi.

Saini________________ Tarehe 31.10.12

Dkt Hezron Mogambi

Saini________________ Tarehe 2/11/2012

Dkt Francis M. Musyoka

# TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia wafuatao:

Kwanza ni babangu Meshack Nyanchama aliyetuaga nilipokuwa ninaendelea kuisomea shahada hii ya uzamili. Alisimama nami tangu nikiwa mchanga wakishirikiana na mamangu Lucia Nyakerario. Walinifanya niwe na ari ya kutia juhudi na kufaulu masomoni. Pili ni mume wangu Francis Onyoni ambaye amenipigania kwa kila namna kuona kwamba nimepiga hatua kimasomo maishani. Tatu ni kwa watoto wangu Christine, Immaculate, Roxanne, Edda na Maryanne ambao walikubali kukaa pekee yao nikiwa mbali masomoni. Nawaombea Mola awaonekanie kwa yote.

# SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Maulana kwa uhai nguvu na afya njema katika kipindi hiki cha miaka miwili nilichochukua kusomea shahada ya uzamili. Pili nawatolea shukurani zisizo na kifani wasimamizi wangu Dkt Hezron Mogambi na Dkt Francis M Musyoka kwa mawazo, ushauri na mwongozo wao kupitia njia za ukweli na kiusomi.

Ningependa kuwashukuru pia wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili ambao walinifunza na kuniandaa vilivyo ili niweze kukabili kazi ya kiutaalamu kiasi hiki. Wahadhiri hasa walionipa ushauri, uelekezi na usaidizi ni pamoja na Profesa John Habwe (mwenyekiti wa idara), Dkt Iribe Mwangi, Dkt Kineene wa Mutiso, Dkt Zaja Omboga, Dkt Mwenda Mbatiah, Dkt Evans Mbuthia, Dkt Jefwa Mweri na Bwana Basilio Mungania katika kozi hii.

Nawashukuru pia wasomi wenzangu ambao tulishirikiana na kushauriana kwa pamoja kuhusu maswala mbalimbali ya kiusomi. Wao ni pamoja na Modgeni Chisia, Sebastian Mutswenje, Ruth Naliaka, Nixon Migiro, Samson Otwere, Pauline Rono, Monica Ruto, David Bore, Rael Onchangu, Janet Mwende, Jackline Kavivi, Bernard Ogolla, Jenifer Okech, Doreen Mboti, Elija Obure, Jones Manoti, Philip Maina, Grace Mjomba, Elsie Gatakaa, Florence Wanjiku, Leah Gatimu, Charles Ndege , Said Omar na Timothy Kiunga.

Shukrani za dhati zamwendea mume wangu Francis Onyoni na watoto wangu kwa kunipa moyo na kujitolea kusimama nami na kunifadhili wakati huu wote nilipokuwa nikisomea shahada hii ya uzamili. Changamoto tulizokumbana nazo kama familia hazikufanya hata mmoja wetu kutingika. Tulikabiliana nazo hadi tamati. Nawaomba mwendelee na moyo huo imara na Mola awabariki.

Mwalimu mkuu na walimu wote wa shule ninapofanya kazi pia nawashukuru sana kwa kunivumilia nilipokuwa ninaenda masomoni pengine wakati mlipokuwa mnanihitaji. Nawaombea Mola awape baraka zake zisizo na kikomo.

Ndugu , dada na pia marafiki zetu wa mbali na karibu siwezi kuwasahau kamwe kwa kuwa mlitufaa kila wakati mlipohitajika kwa kunihimiza na kunisadikisha bila kuchoka. Mlihakikisha kwamba sijakosa malazi, chakula na mahitaji yangu yote nikiwa mbali na kwangu. Kwa yote Mola awashehenezee neema zake sufufu.

# IKISIRI

Utafiti huu ulishugulikia usawini wa wahusika wa kike katika tamthilia za natala na *Mama ee* kwa kutumia nadharia ya ufeministi. Madhumuni ua utafiti huu yalikuwa; Kuchunguza jinsi watunzi walivyowasawiri wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala (2011) na Mama ee (2011)*, Kuchunguza matumizi ya lugha baina na kati ya wahusika katika tamthilia za *Natala* (2011) na Mama *ee (2011),* Kuchunguza mandhari ya usimulizi na usimulizi wenyewe katika tamthilia za *Natala (2011)* na *Mama ee (2011).*

Katika sura ya kwanza tulielezea kwa ufupi maswala ya kimsingi katika utafiti. Tulieleza tatizo letu la utafiti na kuorodhesha madhumuni na nadharia tete za utafiti huu. Katika sura hii pia tulishugulikia sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, misingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii na njia ya utafiti. Tulitumia mbinu ye maktabani katika kukusanya data tuliohitaji na kuichanganua.

Katita sura ya pili tulishugulikia vipengele vya fani katika tamthilia.

Katika sura ya taru tulushughulikia ubabedume na historia yake. Katika sura ya nne nayo tulishughulikia wahusika wa kike katika tamthilia ya *Mama ee* na sura ya tano tukachunguza wahusika wa kike katika tamthilia ya *Natala*.

Katika sura ya sita tulishughulikia muhtasari wa utafiti na mapendekezo ya utafiti.

# YALIYOMO

Ungamo ... i

Tabaruku ... ii

Shukrani ... iii

Yaliyomo ... v

**SURA YA KWANZA: MASWALA YA KIMSINGI KATIKA UTAFITI ... 1**

1.0 Utangulizi ... 1

1.1 Tatizo la utafiti ... 2

1.2 Madhumuni ya utafiti ... 3

1.3 Sababu za kuchagua mada ... 3

1.4 Upeo na mipaka ya utafiti ... 4

1.5 Nadharia tete ... 5

1.6 Misingi ya kinadharia ... 5

1.6.1 Matapo mbalimbali ya ufeministi ... 9

1.6.2 Ufeministi wa kifaransa ... 9

1.6.3 Ufeministi wa kimarekani ... 10

1.6.4 Ufeministi wa kiingereza ... 11

1.6.5 Ufeministi wa kiafrika ... 11

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo ... 12

1.8 Njia za utafiti ... 17

1.9 Hitimisho ... 18

**SURA YA PILI: VIPENGELE VYA FANI KATIKA TAMTHILIA ........................19**

2.0 Vipengele vya fani katika tamthilia ........................................................................19

2.1 Utangulizi....................................................................................................................19

2.2 Dhana ya fani ..............................................................................................................19

2.3 Wahusika.....................................................................................................................20

2.3.1 Uchanganuzi wa wahusika na uhusika katika tamthilia ..................................20

2.3.2 Mbinu za uchunguzi wa wahusika wa tamthilia.............................................21

2.3.3 Suala la ujielezaji wa wahusika ........................................................................22

2.3.4 Njia ya kuwasawiri wahusika katika tamthilia ...............................................23

2.3.4.1 Ulinganuzi wa wahusika ..........................................................................23

2.3.4.2 Mbinu dhahiri za usawiri wa wahusika ...................................................23

2.3.4.3 Mbinu ya matumizi ya majina .................................................................23

2.3.5 Wahusika na usawiri wao ..................................................................................25

2.4 Mandhari ......................................................................................................................26

2.4.1 Sifa za jukwaa ...................................................................................................29

2.4.2 Eneo la uigizaji ..................................................................................................29

2.4.3 Uangazaji wa jukwaa.........................................................................................29

2.5 Lugha ...........................................................................................................................30

2.5.1 Usimulizi ...........................................................................................................31

2.5.2 Usimulizi maizi .................................................................................................32

2.5.3 Usimulizi wa nafsi ya kwanza...........................................................................32

2.6 Mtindo..........................................................................................................................35

2.6.1 Uteuzi wa msamiati ...........................................................................................36

2.6.2 Tamathali za usemi....36

2.6.2.1 Sitiari....37

2.6.2.2 Tashihisi....37

2.6.2.3 Kinaya....38

2.6.4 Kwelikinzani....38

2.6.4.1 Taashira....39

2.6.4.2 Chuku....39

2.7 Hitimisho....40

**SURA YA TATU: UBABEDUME....41**

3.0 Utangulizi....41

3.1 Uana....41

3.2 Ubabedume kama muhimili mkuu wa ugandamizwaji wa wanawake....42

3.3 Historia ya ubabedume....44

3.4 Namna ubabedume hudhiirika katika jamii....48

3.5 Hitimisho....51

**SURA YA NNE: WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *MAMA EE*....52**

4.0 Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *mama ee*....52

4.1 Wahusika....52

4.1.1 Mwavita....52

4.1.2 Kinaya....53

4.1.3 Tenge ....................................................................................................54

4.1.4 Mama....................................................................................................55

4.1.5 Padre....................................................................................................56

4.1.6 Wanakijiji ..............................................................................................58

4.2 Matumizi ya lugha katika tamthilia ya *mama ee* ...............................................60

4.2.1 Uzungumzinafsi........................................................................................60

4.2.2 Mazungumzo baina ya wahusika.....................................................................62

4.2.2.1 Mama na mwavita...................................................................................62

4.2.2.2 Baba, tenge na kaka ...............................................................................63

4.3 Mandhari ya tamthilia ya mama *ee* ...............................................................64

4.3.1 Mandhari ya usimulizi..................................................................................65

4.3.2 Hitimisho ................................................................................................72

**SURA YA TANO: WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA***

**....................................................................................................................73**

5.0 Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *natala*......................................73

5.1 Mandhari ya tamthilia ya *natala* ...................................................................73

5.2 Wahusika katika tamthilia ya *natala*...............................................................78

5.2.1 Tango mwina ............................................................................................78

5.2.2 Natala.....................................................................................................80

5.2.3 Wakene ...................................................................................................81

5.2.4 Mtunza jengo la ufuo ...................................................................................82

5.2.5 Mama lime na tila.......................................................................................83

5.2.6 Gane......84

5.3 Matumizi ya lugha katika tamthilia ya *natala* ......84

5.3.1 Tashihisi ......84

5.3.2 Methali......85

5.3.3 Mchezo ndani ya mchezo ......86

5.3.4 Jazanda ......87

5.3.5 Istiari......88

5.3.6 Kinaya ......88

5.4 Hitimisho......90

**SURA YA SITA: MUHTASARI ......91**

6.0 Tathimini na mapendekezo ......91

6.1 Utangulizi......91

6.2.1 Ushindi wa wahusika wanawake katika tamthilia ya *natala*......91

6.2.2 Ushindi wa wahusika wa kike katika tamthilia ya mama ee. ......94

6.3 Mapendekezo ya utafiti......96

**MAREJELEO ......98**

# SURA YA KWANZA: MASWALA YA KIMSINGI KATIKA UTAFITI

## 1.0 UTANGULIZI

Watunzi wengi wa kazi za sanaa wameshambulia utamaduni unaomfinya na kumnyima mwanamke uhuru wa uamuzi wa mambo yake. Waandishi hao ni kama Ari Katini Mwachofi (1987), Alamin Mazrui (1982), Penina Mlama (1978), Clara Momanyi (2004,2006) na Kithaka wa Mberia (1997). Katika kazi hizi na zingine, wanawake wamepigania usawa kati ya mume na mke katika asasi mbalimbali za maisha. Tamthilia ya Ari Katini Mwachofi (2011) ya *Mama ee* na ya Kithaka wa Mberia (2011) *Natala*, ni baadhi ya nadharia ambazo zimeshughulikia mambo ya wanawake wanaonyimwa haki na kudhulumiwa na wanaume. Watunzi wa kazi hizi mbili wamepiga vita jamii inayomuwekea mwanamke ada nyingi za maisha. Nadharia ya ufeministi imetumiwa kuchanganua kazi zilizoandkwa kabla ya nadharia hiyo kutumiwa katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Waandishi hao pia wamekoleza mielekeo ya kifeministi katika kazi zao ili kuwafundisha umma kuhusu usawa na uwezo wa wanadamu wote. Manufaa muhimu ya nadharia inayozungumzia maswala ya wanawake ni kwamba inapigania usawa miongoni mwa wanadamu na inaonyesha udhaifu wa mfumo dume. Inatetea uhuru wa mwanamke kwa kudai kuwa ana haki ya kupata na kufurahia haki zote za binadamu.

Wafula R.M na Njogu K (2007) kwa upande mwingine nao wanasema kuwa kuna watunzi wanaochuja suala la mama kwa kuzingatia mtazamo wa kisaikolojia. Aghalabu waandishi hao wanaonyesha kasoro zilizomo katika tabia za wanaume ambazo wanaume

hutaka kuficha daima kwa kurejelea sifa wanazo kuwasawiri kuwa wema na wenye kutawala.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Maswala ya wanawake yamezungumziwa kwa mapana na marefu. Baadhi ya watunzi wa maswala ya wanawake wameshambulia utamaduni unaomfinya na kumnyima mwanamke uhuru wa kuamua mambo yake. Katika kazi zao na za wengine, wanawake wamepiga vita waking'ang'ania usawa kati ya mume na mke katika asasi mbalimbali za maisha. Katika kazi nyingi zinazozungumzia wanawake, kumepatikana kuwa, watunzi wengi hawajawatumia wahusika wanawake kama wahusika wakuu. Mara nyingi wanatumiwa kama wahusika wajenzi. Katika tamthilia za *Natala* (2011) na *Mama ee* (2011), wanawake ndio wahusika wakuu. Hii ilichochea sana kuchaguliwa kwa mada hii ili kuchunguza, kuonyesha, na kubainisha mitagusano inayoibuka katika jamii husika na namna ambavyo wahusika wanavyoathirika ndani kwa ndani. Tasnifu hii ni tahakiki ya usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala* na *Mama ee*. Madhumuni yetu ni kuonyesha namna ambavyo watunzi Kithaka wa Mberia (2011) katika tamthilia ya *Natala* na Ari Katini Mwachofi (2011) katika tamthilia ya *Mama ee* walivyowasawiri wahusika wa kike. Yetu ni kutaka kuonyesha namna ambavyo mtunzi alidhamiria kuwasawiri wahusika wa kike na kutokeza msukumo wa matendo yao na hali zao za kisaikolojia. Kutaka kuchunguza na kuhakiki jinsi wanawake ambao wamezinduka wanatetea na kupigania haki zao ili kuwakomboa wanawake kutokana na mateso wanayoyapata kutoka kwa wanaume.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu ni kuhakiki wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala (2011)* na *Mama ee (2011)*. Uhakiki huu unanuia:

i) Kuchunguza jinsi watunzi walivyowasawiri wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala (2011) na Mama ee (2011).*

ii) Kuchunguza matumizi ya lugha baina na kati ya wahusika katika tamthilia za *Natala* (2011) na Mama *ee (2011).*

iii) Kuchunguza mandhari ya usimulizi na usimulizi wenyewe katika tamthilia ya *Natala (2011)* na *Mama ee (2011).*

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Sababu hasa ya kuchagua mada hii,ni kuchunguza na kuonyesha kuwa wanawake wote wanastahili kuzinduka na kushirikiana na wanawake wengine ili kupigania ukombozi wao kutoka kwa utawala wa wanaume wenzao.

Mutua (2007) katika tasnifu yake ya uzamili anasema kwamba kuna harakati nyingi zinazoendelea za kupigania ukombozi, haki na usawa wa wanawake. Uhakiki huu ulikuwa nyenzo madhubuti ya kutolea mchango wetu katika harakati za kumkomboa mwanamke katika jamii.

Ndung'o (1985) asema kwamba ukombozi wa wanawake huwezi kupatikana pasipokuwa na jamii nzima kujihusisha. Utafiti huu ulishughulikia kazi hizi mbili kwa sababu wahusika wakuu katika kazi zote ni wanawake ambao wamesimama wima kutetea haki

zao. Wahusika hao pia wametoka katika mazingira tofauti, na wote wana matatizo kutoka kwa waume wao. Natala ambaye ndiye mhusika mkuu katika tamthilia ya *Natala (2011)* ni mwanamke ambaye ana urembo wa sura na akili. Amesawiriwa kama mhusika wa mazingira ya mashambani na ambaye amewajibika nyumbani kwake. Urembo huo alionao ndio umewafanya wanajamii kumgandamiza kuwa anaasi utamaduni na kufanya mambo kinyume na matakwa ya jamii.

Mwavita ambaye ndiye mhusika mkuu katika tamthilia ya *Mama ee (2011)* ni kielelezo kwa wanawake wengine katika jamii. Amesawiriwa kama mhusika wa mazingira ya mjini na anafanya kazi ya serikali. Kinaya ambaye ni mumewe anafanya kinyume na matakwa ya familia kwa kujitumbukiza katika dimbwi la ulevi na uasherati na kusahau familia yake. Amewacha wajibu wake kwa sababu mkewe anafanya kazi, hivyo anaweza kugharamia mahitaji yote ya nyumbani. Kinaya anapofika nyumbani usiku anashusha ugomvi, na kumpiga Mwavita jambo ambalo linasababisha kumn'goa meno na hata kuavya mimba. Dhuluma na mateso ya wanaume kwa wanawake huwaathiri wanawake bila kujali umri, cheo, waliosoma na wale ambao hawajasoma. Hiki kilituchochea sana katika uchaguzi wa mada hii ili wanawake watakaosoma kazi hii waweze kuzinduka na kupigania haki na ukombozi wao katika dunia hii inayotawaliwa na wanaume.

## 1.4 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu ulijifunga kwenye kipengele kimoja cha fani cha wahusika ambapo ulichuchunguza jinsi wahusika wa kike wanavyosawiriwa katika tamthilia za *Natala (2011)* na *Mama ee (2011).* Ulichunguza matumizi ya lugha baina ya wahusika

mbalimbali. Ulichunguza jinsi mtunzi ameteua mtindo wake wa lugha na jinsi mtindo huu unavyowaathiri wahusika wa kike. Ulichunguza pia jinsi mandhari ya usimulizi yanavyowabagua wanawake. Kazi hii ilijikita katika kuchunguza jinsi mtunzi anavyowasawiri wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala (2011)* na *Mama ee(2011).*

## 1.5 NADHARIA TETE

i) Wandishi wamewasawiri wahusika wa kike kwa njia hasi na chanya jambo ambalo limechangia pakubwa ukuaji wa tamthilia za *Natala* (2011) na *Mama ee* (2011)

ii) Lugha inayotumika katika tamthilia ya *Natala* na *Mama ee* imewabagua wahusika wa kike.

iii) Mandhari na usimulizi katika kazi hizi vinawabagua wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala* na *Mama ee*.

## 1.6 MISINGI YA KINADHARIA

Nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu na kuvielewa katika vipengele vyake vyote. Ni mtazamo fulani kuhusu uhalisi wa maisha ya mwanadamu. Utafiti huu umejikita katika nadharia ya ufeministi. Nadharia hii ya ufeministi inachunguza na kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu maswala ya wanawamke katika jamii kwa kutumia nadharia ya ufeministi kwa jumla. Utafiti huu ulitumia tapo moja la nadharia ya

ufeministi ambalo ni Ufeministi wa Kiafrika. Tapo hili la ufeministi huzungumzia juu ya wanawake wa Kiafrika jinsi wanavyosisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomfinya na kunaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake.

Kimsingi hii ni nadharia ambayo inaweka misingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Wanawake wemekuwa wakipigania haki zao katika kipindi chote ambacho binadamu ameitawala sayari hii. Maswala ya kiufeministi yalianza kuzungumziwa katika karne ya kumi na tisa na kuanza kutia fora katika miaka ya sitini na sabini ya karne ya ishirini ambapo wanawake hasa wa kimagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao kwa utaratibu yaani katika machapisho. Kabla ya kuanzishwa kwa nadharia hii kulikuweko na jitihada mbalimbali za kupigania usawa baina ya wanawake na wanaume. Katika nchi ya Ufaransa mnamo miaka ya (1789-1795) katika kilichojulikana kama "Msimbo wa Nepoleon" (Code of Nepoleon) ambapo wanawake waliandamana kukataa kushushwa kwa hadhi yao. Pale, Nepoleon alisema kuwa akili za wanawake ni dhaifu ukizilinganisha na za wanaume. Kwa hivyo walifaa kupewa elimu ya kiwango cha chini na kazi zao kuwa za viwango vya chini kama ushonaji.

Katika Marekani Kaskazini, wanawake kama Abigail Adam na Mercy Otis Warren walitaka George Washington na Thomas Jefferson kuongeza ukombozi wa wanawake katika kipengele cha katiba ambapo haikufua dafu. Mnamo mwaka wa (1848) kuna kundi la wanawake walioungana ili kuleta ukombozi wa wanawake. Mkutano wao ulifanyika kule New York ambapo walitangaza matokeo yao ya wanawake kuwa huru.

Matokeo yao nayo ni, kuwa wanawake; kukubaliwa kupiga kura, wapewe usawa wa kisheria, wapewe masomo ya kutosha, wapewe nafasi sawa ya kufanya biashara, wapewe usawa wa kupata fidia na wapewe haki za kupata ujira.

Dora na Webster (1925) wanaeleza kuwa, katika ulimwengu wa leo, ugomvi katika ndoa ni mwingi kiasi kwamba inahusisha makundi makubwa ya jinsia na matabaka yote ya jamii. Webster anazidi kufafanua ya kwamba dharau kwa mwanamke inaonekana wazi kwani mara nyingi mtu akihusishwa na mwanamume hujihisi kuwa na hali chanya ilhali akihusishwa na mwanamke hujihisi kuwa na hali hasi. Ni heshima kuu mtu kuwa mwanamume na akiwa mwanamke ni aibu tupu.

Webster (1970) akiuelezea msimamo wa mwandishi maarufu wa maswala ya kiufeministi Virginia Woolf katika kazi yake *A room of one's own* (1928) kuwa; ukosefu wa waandishi wa kike unatokana na hali zao za maisha, kwa kukosa uwezo wa kifedha na kwa jumla wanahitaji kuhudumia mahitaji ya wanaume wao.

Tuttle (1986:107) naye anasema kuwa ufeministi unaibuka kutokana na madai kwamba kuna dosari kwa namna ambavyo jamii inavyomchukulia mwanamke.

Ogundipe (1994) ana maoni kwamba wanawake wamepewa majukumu dunifu na yanayosawiriwa kwa ubaya kama vile uchawi na wanaume nao kusawiriwa kama werevu, wenye nguvu, wa kuaminika na wenye uongozi kwa kuzaliwa. Hali kama hii huchangia kumdunisha na kumtesa mwanamke katika jamii.

Mbatiah (2001) naye alitoa mchango wake kuwa, nadharia ya ufeministi ni kazi ya kifasihi ambapo lengo lake kuu ni kuleta haki za wanawake dhidi ya ugandamizwaji katika jamii iliyo na mfumo uliodhibitiwa na wanaume.

Wamitila (2003) anaelezea nadharia ya ufeministi kama nadharia iliyowekewa misingi katika kupigania ukombozi wa wanawake dhidi ya pingu za kiutamaduni, kidini na kijamii. Nadharia hii inachunguza itikadi ya kiume ambayo imekuweko katika kipindi kirefu. Pia hushambulia mtazamo wa kiume kuhusu namna wanawake wanavyotarajiwa kuishi.

Njogu na Chimerah (1999) nao wanakinzana na mikabala ya kiumeni ambayo huonekana kuwapendelea wanaume na kuwabagua wanawake. Kulingana na Chimerah nadharia hii ina sifa maalumu kama vile: Nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa kuelezea kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi. Mtazamo huu vilevile unajaribu kuwahamasisha watungaji wa kazi za sanaa ili wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo wenye uwezo na ambao wanaweza kuigwa na wanawake wengine. Wahusika hao watakuwa na nguvu za kijamii na wasiotegemea wanaume kujitambulisha. Pia kisaikolojia wawe ni wanawake wanaojielewa na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wana udhalifu kwa ajili ya umenge wao. Nadharia hii inanuia kuwasawasisha watu wote kwa upande wa utamaduni wa kimenke. Inapigania jamii mpya yenye misingi katika amali za kibinadamu bila kujali maumbile. Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Wanawake wanahimizwa kupana nguvu. Mtazamo huu una shabaha ya kuamusha na

kuzindua mwamko miongoni mwa wanawake ili wawe watendaji zaidi na washiriki ipasavyo katika ukombozi wao wenyewe.

Mkabala huu unatilia mkazo kauli za utendaji wala sio za kimapokezi. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kuvumbua na kuweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume. Inanuia pia kuchunguza historia ya kifasihi ya jadi ya kike, na kuwamulika waandishi wa kike waliotambua hali za wanawake na ambao wanaweza kuchukuliwa kama vielelezo kwa wasomaji wao.

### 1.6.1 MATAPO MBALIMBALI YA UFEMINISTI

Nadharia ya ufeministi imegawika katika matapo mbalimbali kama tunavyoarifiwa na Wafula R na Njogu K (2007:92-93) Tangu nadharia hii ilipochipuka, kuna njia mbili kuu za kubainisha matapo yake. Njia moja ni ile inayozungumzia maswala ya wanawake kimaeneo, na nyingine ni ya msistizo na mielekeo maalum katika nadharia ya ufeministi. Wahakiki walioainisha fasihi kimaeneo ni Mary Eagleton (1991) na Ross Murfin (1991) ambao waligundua kuwa kuna matapo manne ya ufeministi, nayo ni pamoja na Ufeministi wa Kifaransa, Ufeministi wa Kiingereza, Ufeministi wa Kimarekani, na Ufeministi wa Kiafrika.

### 1.6.2 UFEMINISTI WA KIFARANSA

Wanawake wa Kifaransa wanatilia lugha mkazo. Utafiti wao unalenga katika kufafanua namna lugha inavyomtolea maana mtumiaji wake. Wanadai kwamba lugha kama

inavyotumika ni zao la taasubi ya kiume. Inampendelea mwanamume zaidi kuliko mwanamke. Jazanda za kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka ni za kiume ilhali zile za kusawiri ulegevu na kutoweza ni za kike.

### 1.6.3 UFEMINISTI WA KIMAREKANI

Huu unahusishwa na kazi ya Mary Ellman (1968) *Thinking About Women.* Dhamira ya kimsingi ya mwandishi huyu ilikuwa ni kuangaza jinsi wanawake walivyosawiriwa kwa namna mbalimbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwandishi huyu alimulika jinsi baadhi ya waandishi wa kike wanavyoendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Hali hii ilitokana na wao kukalia kwenye jamii inayotawaliwa na itikadi za kiume na kuishia kufyonza baadhi ya mitazamo kumhusu mwanamke ambayo inaakisiwa kwenye kazi zao.

Kitabu cha Betty Freidan: *The Female Mystique* (1963) kinachukuliwa kama kichocheo kikubwa kwa kuzuka kwa hisia za kifeministi wa Marekani. Friedan anayachunguza maisha ya wanawake ambao kwa kiasi kikubwa ni mzingile sio tu kwa wanaume bali pia kwa wanawake wenyewe. Mwandishi anaendelea kusema kuwa kuyaelewa maisha hayo kumebakia msingi mkubwa wa hali ya maisha ya wanawake kijumla. Mwandishi mwingine ambaye amekuwa na athari kubwa katika historia ya ufeministi ni Kate Millet aliyeandika kitabu cha *Sexual Politics* (1979). Hii ni kazi inayoshambulia vikali baadhi ya waandishi maarufu wa kiume kutokana na jinsi wanavyowasawiri wahusika wao wa kike. Waandishi waliochunguzwa na Millet ni D.H. Lawrence, Henry Miller, Norman Mailer na Jean Genet. Millet anabainisha kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake

inashirikiana kumkandamiza mwanamke. Pili mwandishi huyu anaushambulia mkabala wa saikolojia changanuzi unaohusishwa na Sigmund Freud kwa kuwa na upendeleo mkubwa wa mfumo wa ubabedume. Freud (1950) alisema kuwa mtoto wa kike anaanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume (wivu wa zubu). Millet anasema kuwa wivu uliopo ni uwezo alionao mwanaume kutokana na muundo wa kijamii. Mwanamke anakua na wivu wa kinachoashiriwa na hicho kiungo. Wanakubaliana na Wafaransa kuhusu lugha. Wanaongeza kwamba, wanawake wana namna yao ya kipekee ya kuandika na kujieleza. Wanasema pia kuwa kuna dhamira zinazorudiwa katika tungo za wanawake.

### 1.6.4 UFEMINISTI WA KIINGEREZA

Wanafikiria kuwa wenzao wa Kimarekani wanazungumzia zaidi maswala ya kihisia na kisanaa na kusahau historia ya kisasa. Kwao mambo ya kihistoria na kisiasa ndio huathiri matendo ya wanawake. Kimya cha kulazimishwa na pia desturi na mila zinazomdhalalisha mwanamke kama vile kuonewa kwa mwanamke asiye na uwezo wa kuzaa.

### 1.6.5 UFEMINISTI WA KIAFRIKA

Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomfinya na kumnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vyaUfeministi wa Kiafrika ni; Kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketaji wa wanawake, desturi na mila zinazomdhalalisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiye na uwezo wa kuzaa.

Millet (1977) anasema kwamba ufeministi wa Kiafrika umetokana na utamaduni katika jamii iliyojikita katika kilimo na ushirikiano wa kijamii. Umejengeka katika misingi thabiti ya kumhusisha mwanamke katika shughuli tofauti za jamii bila kuangalia asasi zinazotawaliwa na wanaume. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza usawa katika shughuli za jamii na utoaji uamuzi kwa wanawake na wanaume.

Strobel (1980) anauona ufeministi wa Kiafrika kama ambao umekumbana na changamoto nyingi kutokana na asasi tofauti kwa sababu huwa unataka kujua chanzo cha ubaguzi katika maswala ya kiutawala. Mwelekeo pinzani unasisitiza uongozi wa jinsia ya kiume ambao umeipa changamoto nyingi sana mwelekeo wa ufeministi wa Kiafrika.

Steady (1981) anaunga mkono ufeministi wa Kiafrika. Anaueleza kuwa unaojikita kwenye misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanavyotegemeana na kukamilishana, yenye usambamba na usawa katika kuendeleza jamii. Anasema kuwa ufeministi wa Kiafrika unaweka pamoja maswala ya ubaguzi, uana, utabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuleta ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe lakini sio kama kiumbe kijinsia. Anaendelea kusema kuwa ufeministi wa Kiafrika unaangalia maswala ya kiutamaduni yanayomlemaza mwanamke. Unashughulikia maswala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Tafiti kuhusu usawiri wa wanawake na watunzi mbalimbali halikuanza jana bali ni mambo ambayo yamekuwepo tangu jadi. Baadhi ya kazi za mwanzomwanzo

kuyafafanua maswala ya wanawake kinadharia zilikuwa *A Vindication of the Rights of Women,* Mary Wollstonecraft (1792) na *A Room of Ones Own* Virginia woolf, (1929). Mary Wollstonecraft ndiye anayefahamika kuwa mtalaamu wa kwanza kuyazungumzia maswala ya wanawake kwa utaratibu maalumu. Mary anadai kwamba mielekeo hasi kumhusu mwanamke imesababishwa na elimu mbovu wanayopewa wanawake na wanaume. Chapisho lililochangia pakubwa zaidi katika maendeleo ya uhakiki wa nadharia hii ni *The Second Sex* (1952) ambalo ni la Mfaransa Simone de Beauvior. Lengo lake kuu lilikuwa kubainisha, kukosoa na kuzipiga vita asasi zinazomdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Asasi hizo alizitaja kama dini, ndoa na utamaduni. Aliendelea kusema kuwa dini humfunza mwanamke kunyenyekea. Ndoa nayo imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamke. Utamaduni nao humsawiri mwanamke katika tamathali hasi na duni.

Germane Greer katika kitabu cha *The Female Eunuch* (1981) anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa inawafanya wanawake kumilikiwa na kukosa ubinafsi na uhuru wao. Wengine ambao wametoa mchango wao ambao wanazungumza juu ya maswala ya mwanamke ni wengi. Wao wamepigania usawa kati ya mume na mke katika asasi mbalimbali za maisha. Katika tamthilia ya Ari Katini Mwachofi (1981) ya *Mama ee* inakusudio mkubwa wa wanawake wanaonyanyaswa. Mwachofi amepiga vita jamii inayomuwekea mwamke majukumu mengi yanayomzuia kujiendeleza katika nyanja nyingi za maisha.

Lugano (1989) ametafiti usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kijamii katika riwaya tatu za Kezilahabi. Katika riwaya hizo ameonyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama mtegemezi wa mwanaume, chombo chake na chanzo cha maovu yote. Utafiti wake unaegemea riwaya lakini wetu umeegemea tamthilia. Utafiti wake umetufaa kwa sababu unatupatia picha iliyopo kwa sasa kumhusu mwanamke. Picha hiyo imetusaidia kwa kulinganisha tanzu hizo mbili.

Osiemo Dio (1997) ameangalia fani katika diwani mbili ili kutathmini thamani ya fani iliyotumiwa. Ameangalia mchango wa kila kipengele cha fani katika kujenga umbo imara lililotangamana na fani. Yeye amejikita katika ushairi lakini sisi katika utafiti wetu tumechunguza tamthilia. Uchanganuzi wake wa kifani unatufaa kwani tumejaribu kutumia baadhi ya vipengele vyake na jinsi vinanvyowasawiri wahusika wanawake.

Kiango S (1997) Ametafiti taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Kwa ujumla anasema kuwa kwenye tamthilia zote, mwanamke ameonyeshwa kama asiye sawa na mwanaume. Amesawiriwa kama mbaya, msinifu na muuaji. Yeye anashughulikia tamthilia nyingi kwa jumla, sisi tumeshughulikia mbili na kuzichanganua kwa undani.

Kruger (1998) naye ametafiti kuhusu usawiri wa wanawake kulingana na waandishi wa Kiafrika walioandika riwaya na hadithi fupi. Anasema kuwa waandishi hawa hawatumii wahusika wanawake kama wahusika wakuu lakini mara nyingi huwatumia kama wahusika wajenzi. Yeye alishughulikia riwaya na hadithi fupi lakini sisi tumeshughulikia

tamthilia pekee. Pia tunapata picha ya waandishi wa Kiafrika vile wanavyowasawiri wanawake katika kazi zao.

Clara Momanyi (1998) ameshughulikia usawiri wa mwanamke muislamu wa jamii ya waswahili. Katika uhakiki wake, Momanyi ameshughulikia *Utenzi wa Mwanakupona*. Yeye amemsawiri mwanamke kama amedunishwa. Anasema kuwa sababu inayompelekea mwanamke kudunishwa ni dini ya kiislamu. Kazi hii ni muhimu katika kazi yetu kwa sababu imetusaidia kuangaza zaidi jinsi dini inavyochangia kudunishwa kwa mwanamke. Dini ni mojawapo ya asasi zinazoendeleza mfumo wa ubabedume ambao humdunisha mwanamke.

Wepo Wasa (2005) amefanya uhakiki wa fani katika utenzi wa *Siri li Asirali* na utenzi wa *Fatuma*. Katika tasnifu yake ameshughulikia fani katika tenzi hizi mbili. Kazi yake imetusaidia kulinganisha matumizi ya fani baina ya uandishi wa kitambo na wa hivi sasa. Katola (2006) katika tasnifu yake ya uzamili anaendeleza kwamba kuna udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za kiswahili. Anaendelea kusema kuwa kudharauliwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukanwa na jamii ni mambo ambayo yamejitokeza katika jamii zetu.

Mutua J. (2007) Ametafiti mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa wanawake *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (S. Mohamed), katika utafiti wake amebainisha iwapo vijana na wazee kwa ujumla wanaunga mkono au wanapinga ukombozi wa mwanamke. Utafiti wake unashughulikia mitazamo ya makundi nasi

tumetumia mtazamo wa mwandishi kuhusu wahusika mahususi. Utafiti huu umetufaa kwa sababu umetupatia maoni ya jumla ya wazee na vijana.Pia wametupatia picha ambayo imetusaidia kuelewa kuwa iwapo waandishi tunaojishughulisha na tamthilia zao kama wanaunga mkono ukombozi wa wanawake au wanaupinga. Tumetazama pia jinsi wahusika vijana au wazee wanavyotumia lugha wanapolenga mhusika mwanamke. Hii hutusaidia kuelewa ni kwa nini wanawachora wahusika wanawake jinsi wanavyowachorwa katika tamthilia zao kwa kutumia lugha.

Wamitila (2007) katika mwongozo wa *Mwisho wa Kosa* anasema kuwa ndoa imepewa sura mbili: Ndoa ya kitamaduni ambayo hupangwa na wazazi ambapo mwanamke hupangiwa mwanaume wa kumuoa bila yeye kupanga wala kusema lolote, na ndoa ya kisasa ambapo wachumba hujichagulia mtu wa kumuoa. Hapa mwanamke na mwanaume hupanga mambo yao ya ndoa. Ni jukumu lao kuwafahamisha wazazi kuhusu mipango yao au la.

Kazi ya Wamitila ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu imetusaidia kuchunguza utamaduni na usasa kwa undani na kujaribu kuona ni wapi mwanamke amekandamizwa zaidi.

Mulila J. (2007) naye ameangalia usawiri hasi wa wahusika wanawake katika tamthilia za *Zilizala na Chamchela.* Ameshughulikia mchango wa wasanii katika vita vya kumkomboa mwanamke kutokana na minyororo ya utumwa ukiwemo usawiri hasi na kuibadilisha jamii imuone mwanamke kwa namna tofauti na vile inavyomuona.

Anaangalia pia jinsi wahusika wanawake na wahusika wanaume wanavyochangia katika kueneza picha hasi ya wanawake, pia anachunguza itikadi hasi kumhusu mwanamke. Ameangalia mchango wa wahusika wanawake katika ukombozi wao na sifa chanya katika tamthilia hizi zilizoandikwa kwa uchanya kuhusu mwanamke.

Katika kazi hii utafiti huu umetumia mchango wake kukamilisha jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia za *Natala (2011)* na *Mama ee (2011*).Katika kazi hizi mbili wanawake wamezinduka na kuamua kupigania ukombozi wa wanawake wote. Katika tamthilia ya *Natala*(2011)Natala amepambana na vizingiti vingi katika juhudi zake za kumkomboa mwanamke dhidi ya ubabedume na hatimaye anafaulu kumpokonya Wakene cheti cha shamba nakumchapa kwa kutumia kikaango hadi pale wanapokutana na Tango kwa mlango na kudhani kuwa ni mzuka.Katika tamthilia ya Mama ee wahusika wanawake hasa Mwavita na Tenge wana nia ya kuchengua ulimwengu wa kimapokeo na kuufinyanga ulimwengu huo upya.Kutokana na dhuluma walizozipitia katika sehemu ya kwanza ya tamthilia walidhamiria kuwakomboa wanawake wenzao kwa kuwaelimisha jambo ambalo lilibidi wazushe rabsha na fujo ili waweze kufikia nia yao.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Tasnifu ambazo zimeshughulikia nafasi ya mwanamke katika jamii ziliweza kupitiwa na zikawa za manufaa sana.Nadharia ya ufeministi ambayo utafiti huu umetumia pia ilisomwa. Vipengele vya fani ambavyo tumevichunguza ni pamoja na matumizi ya lugha baina ya wahusika, wahusika wenyewe, tumeshughulikia mandhari na usimulizi katika tamthilia mbili; *Natala* (2011) na *Mama*

*ee (2011).* Pamoja na hayo, utafiti huu umechunguza tapo la nadharia ya ufeministi ambalo lilitumika katika kufanya utafiti huu ambao ni ya Ufeministi wa Kiafrika kwa undani.

## 1.9 HITIMISHO

Katika sura ya kwanza tumejadili juu ya maswala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti wetu. Maswala hayo ni pamoja na; utangulizi, tatizo la utafiti, sababu za kushughua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, yalioandikwa kuhusu mada hii, misingi ya kinadharia, njia za utafiti na hatimaye hitimisho. Katika sura ya pili tumeshughulikia dhana ya fani, lugha, wahusika, mtindo, usimulizi na mandhari.

# SURA YA PILI: VIPENGELE VYA FANI KATIKA TAMTHILIA

## 2.0 VIPENGELE VYA FANI KATIKA TAMTHILIA

## 2.1 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza tulichunguza maswala ya kimsingi yanayohusu utafiti wetu. Katika sura hii utafiti huu unashughulikia vipengele vya fani, ambavyo vinalenga tamathali za usemi katika tamthilia za *Natala (2011) na Mama ee (2011).*

## 2.2 DHANA YA FANI

Msokile M. (1993:79) anasema kuwa fani ni muundo, ufundi au umbo wa kazi ya sanaa. Anaendelea kusema kuwa fani imegawika katika matawi mbalimbali, kuna fani ya tamathali, fani ya nyimbo, na nyingine nyingi.

Mbatia (2001), anasema kuwa dhana hii ya fani imegawika katika sehemu mbili kuu ambazo ni maudhui na fani. Anasema kuwa maudhui ni maswala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Kwa upande mwingine fani huwa ni vipengele vya kisanii vinavyotumiwa kuwasilisha maudhui.

Wamitila (2002:41), anasema kuwa fani hutumiwa kuelezea muundo wa kazi fulani za kifasihi pamoja na sehemu zake. Umbo lenyewe laweza kuwa la nje au la ndani. Hujengwa kwa vipengele kama vile utangulizi, kati na mwisho.

Njongu K.na Wafula R.M (2007:102) Wanasema kuwa kazi ya kifasihi ni vitengo vya sanaa kama vile, maudhui, ploti, wahusika, matumizi ya lugha.

Wamitilia (2008:345) anasema kuwa fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa kuwasilisha maudhui. Fani huwa njia kuu ya kuwasilisha maudhui. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu wahusika ni kipengele cha fani na hilo ndilo lengo letu la utafiti. Vipengele vya fani ni vingi, katika utafiti wetu vile ambavyo tumevitmia ni pamoja na wahusika , usimulizi, matumizi ya lugha pamoja na mandhari. Tumevitumia kuona vile wahusika wa kike wamesawiriwa kwa ujumla katika tamthilia za *Natala* na *Mama ee.*

## 2.3 WAHUSIKA

### 2.3.1 UCHANGANUZI WA WAHUSIKA NA UHUSIKA KATIKA TAMTHILIA

Maoni ya Wamitilia (2008) ni kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi. Pili wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na matendo na mazungumzo yao jukwaani.

Wahusika wanadhihirishwa na kukuzwa vyema kwa matumizi ya lugha na mazungumzo. Kulingana na maelezo ya Aristotle kama anavyoelezea Wamitilia katika uchunguzi wa wahusika ni kuwa, Aristotle alizuka na kanuni nne muhimu kuhusiana na wahusika wa kifasihi. Kanuni hizi zinakuwa kama msingi wa kuwachunguza na kuwatathmini wahusika hao. Aristotle alisema kuwa, lazima mhusika awe na uthabiti unaotokeza waziwazi, sifa zinazomtambulisha kama mhusika na anayefanana na watu halisi katika

ulimwengu huu wa ubunifu, apewe sifa au vitambulishi vinavyohusiana vizuri na matendo yake na apewe ukwezo fulani wa kimaadili.

### 2.3.2 MBINU ZA UCHUNGUZI WA WAHUSIKA WA TAMTHILIA

Kuna njia mbalimbali za kufafanua na kuhakiki wahusika katika tamthilia. Hata hivyo ni muhimu kuchunguza namna wahusika wanavyosawiriwa na namna wanavyochangia katika uendeleshaji wa tamthilia.

Kulingana na Wamitila (2008), kimsingi tunaweza kubainisha wahusika wakuu na wahusika wadogo. Uainishaji huu unategamea jukumu la kila mhusika katika msuko wa tamthilia hiyo. Sifa zifuatazo ni muhimu katika uchunguzi wa wahusika wa tamthilia.

Kwanza, mhusika yeyote yule ana nafasi katika tamthilia ambapo wahusika wakuu hutokeza mara kadhaa na kwa hivyo huwa na upana anapolinganishwa na wahusika wadogo. Wahusika wadogo hutumiwa kuwajenga wahusika wakuu.

Pili, wahusika na utanzu ni sifa nyingine ya kuwachunguza wahusika katika tamthilia. Aristotle alishikilia kuwa wahusika wa tanzia huwa na hadhi kubwa kijamii ili kuhalalisha anguko lao baadaye ambalo hutokana na udhaifu wao kama binadamu.

Tatu, ni sifa jingine ya kiuchunguzi ni ya umakundi wa wahusika. Katika usomaji wa tamthilia inawezekana kubainisha waziwazi ni wahusika wepi ambao wamejumuishwa

pamoja, ni wahusika wepi marafiki, ni wahusika wepi ambao ni maadui na ni wahusika wepi ambao wako katika upande wa nguli na ni wepi walio katika upande wa upinzani. Nne, wahusika na usemi ni sifa inayohusu usemi au lugha inayobainishwa kama wahusika binafsi. Je! Unapowachunguza wahusika katika tamthilia fulani, wamepewa lugha inayowatenga na wenzao? Hali hii inaweza kupatikana katika matumizi ya sentensi, mtindo rasmi na matumizi ya lugha ya kishairi.

Tano, ni ulinganuzi wa wahusika ni uchunguzi ambao mhusika mmoja ni kinyume na mhusika mwingine. Ulinganuzi huu waweza kuangaza maswala yanayoendelezwa na mhusika, mwelekeo wake na hata mavazi yake.

### 2.3.3 SUALA LA UJIELEZAJI WA WAHUSIKA

Tamthilia inategemea matendo zaidi kuliko maelezo. Jinsi ya kujieleza hutokea kwa njia ya lugha au viziada vya lugha anavyovitumia mhusika ili aweze kueleweka vyema. Ujielezaji huu ni wa aina mbalimbali. Ule wa wazi ambapo wahusika hutamka maneno au kauli ambazo zinawaelezea maoni. Katika hali hii mhusika anajiieleza kujihusu mwenyewe kwa kutumia uzungumzi nafsi mdokezo. Ujielezaji mdokezo ni pale ambapo mhusika hujieleza bila kudhamiria. Katika aina hii njia mojawapo inayotumiwa kama msingi wa ujielezaji ni matumizi ya ishara. Na ishara zinaweza kuwa za uso, mwili, mshuko au mpando wa sauti kwa njia ya uigizaji.

## 2.3.4 NJIA YA KUWASAWIRI WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA

### 2.3.4.1 ULINGANUZI WA WAHUSIKA

Mbinu hii hutumika kuwasawiri wahusika katika tamthilia. Mhusika mmoja huwa na sifa za kinyume akilinganishwa na wahusika wengine, au mhusika mmoja anaweza kuwa na tabia za kutambulika zaidi kuliko wahusika wengine. Tena wahusika wengine ni wanawake na wengine ni wanaume. Sifa hii hufanya wasifu wa wahusika wengine kuwa wazi zaidi.

### 2.3.4.2 MBINU DHAHIRI ZA USAWIRI WA WAHUSIKA

Haya ni maelezo yanayoweza kubainisha mhusika nguli na mhusika hasidi. Msomaji anapata kuelewa sifa hii hata kabla ya kuanza kusoma tamthilia inayohusika. Hii hupatikana katika orodha iliyopo mwanzoni mwa wahusika waliopo katika tamthilia.

### 2.3.4.3 MBINU YA MATUMIZI YA MAJINA

Mtunzi anaweza kutumia majina ambayo yanachangia pakubwa katika kuyaendeleza na kuyakuza maudhui katika kazi husika. Inategemea mtunzi wa tamthilia anataka kutuelekeza wapi. Majina haya yanaweza kutuelekeza kwenye msimamo wake, mwelekeo wake, itikadi yake, maoni yake na hata hisia zake kuwahusu wahusika wengine. Majina yana mchango mkubwa katika uhusika wa wahusika wa kifasihi.

Kulingana na Forster (1927) Wahusika wako katika makundi mawili. Wahusika bapa na wahusika duara. Wahusika bapa huwa hawabadiliki tangu mwanzo hadi mwisho na huwa katika makundi mawili pia. Kuna wahusika bapa sugu ambao hujulikana kutokana

na maelezo ya msanii. Pia tuna wahusika bapa vielezo. Hawa hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo yao. Majina yao huwa kama kifupisho cha wasifu wao. Wahusika duara nao hukaribiana na binadamu wa kawaida. Wao hubadilika kulingana na vile anavyokumbana na mambo, kisaikolojia, kijamii na kisiasa.

Aristotle (1965) alisema kuwa mhusika lazima aonyeshe hali ya juu ya kimaadili, apewe sifa zinazomtambulisha vizuri na matendo yake kama mhusika na uthabiti ulio bayana. Kulingana na maelezo ya wataalamu ni dhahiri kuwa kila mhusika awe na jukumu lake maalumu katika kazi ya kifasihi. Yeye hushikilia kazi yake ili kutimiza malengo ya msanii na nia ya kumfanya kuwa kielelezo katika jamii. Mhusika husawiriwa kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kihalisia.

Wamitila (2004) anaeleza kuwa wahusika tunaokumbana nao katika tamthilia ndio tunaowaona katika riwaya. Hata hivyo zipo tofauti ndogo na muhimu sana. Wahusika ni muhimu katika tamthilia kwa sababu ndio nguzo kuu ya matendo ya kidrama. Anaeleza kuwa mambo ya kuzingatia kuhusu wahusika wa tamthilia ni mazungumzonafsi ambayo ni njia mojawapo inayotumiwa na wahusika wa kifasihi kuyawazilisha mawazo yao ya ndani. Kuna pia matumizi ya usemaji kando ambapo mhusika mmoja anasema maneno kwa hadhira au mhusika mwingine na wenzake jukwaani wanajifanya kuwa hawasikii. Hii ni mbinu muhimu ya kufichua msimamo wa mhusika mmoja kumhusu mwingine. Wahusika wazuri sio wale wanaofanana na watu halisi bali wanaokubalika katika muktadha wa tamthilia na ulimwengu wa ubunifu, wanaoendeleza tendo kuu vizuri na kuwaaminisha wasomaji au hadhira. Wahusika wa tamthilia huweza kukuzwa vyema

kwa kuwepo kwa kinyume cha mhusika mmoja. Njia moja nzuri ya kuufanya wema ujitokeze vyema na kuonyesha ubaya huu ni ulinganuzi. Aghalabu wahusika hupewa lugha ambazo zinawabainisha kama wahusika binafsi. Mwandishi anaweza kutumia mhusika msiri au mfoili kumwendeleza mhusika fulani. Mhusika mfoili ni mhusika ambaye hana jukumu jingine wazi isipokua kutumiwa kuzua mazumgumuzo na mhusika fulani. Muhimu ni kumfanya aonyeshe hisia zake za ndani.

Wahusika wa tamthilia hukuzwa kwa kutegemea matendo kuliko usimulizi wa mwandishi unaopatikana katika tawi kama riwaya au hadithi fupi. Kuna umuhimu wa kulichunguza jukumu la wahusika wa aina hii kabla ya kutoa kauli ya kijumla kuwahusu. Sambamba na kipengele hiki, mwandishi anaweza kuyatumia majina yanayotuelekeza kwenye tabia ya wahusika. Hii ni mbinu ya majazi ambayo tulikumbana nayo huko nyuma.

### 2.3.5 WAHUSIKA NA USAWIRI WAO

Wamitila (2002) asema kuwa kuna njia kadhaa za kuwasawiri wahusika, nazo ni kama ifuatavyo: Kuna mbinu ya uzumgumzinafsi ambayo ina majukumu kadhaa katika tamthilia. Kwanza, inaweza kutumiwa kuyamulika mawazo na hisia za ndani za mhusika anayehusika. Pili, hutumiwa kutudhihirishia mivutano ya ndani kwa ndani aliyo nayo mhusika fulani. Tatu, hutumiwa kuwaendeleza wahusika wa aina fulani hasa wanafiki ambao vinginevyo ingekuwa vigumu kuwaendeleza. Nne, huendeleza msuko wa tamthilia. Uzungumzi huu unamhusu mtu mmoja. Mhusika anayezungumza hapa husema mambo ya kibinafsi, na kwa njia hii hadhira inapata fursa ya kuyajua mawazo

yake kibinafsi. Anaweza kuzungumza kwa kutumia nafsi ya kwanza 'mimi' na akitaka kutoa maoni ya watu wengi hutumia" tu" pia hufika mahali anapojizungumzia kwa kutaja jina lake kama kwamba ni mtu mwingine, hapa hutumia nafsi ya tatu "yeye".

Matendo ya wahusika katika tamthilia ni msingi mkubwa wa kuzifahamu tabia na wasifu wa wahusika. Mwandishi anatumia mbinu hii kuwakuza wahusika mbalimbali kwa njia tofautitofauti. Katika kazi ya tamthilia kuna mahali wahusika wanaweza kutangulizwa hata kabla ya kutokeza jukwaani. Pia kuna uwezekano kukaweko na utangulizi ambao unatuangazia maswala kadhaa kuhusiana na wahusika hao au hata akaweko msimulizi.

## 2.4 MANDHARI

Gills (1985) inasema kuwa mandhari ni neno pana sana linalojumlisha mahali ambapo wahusika wamesawirishwa, muktadha wa jamii, wahusika kama vile familia, marafiki, ndugu, matabaka, tamaduni, imani na kaida za jamii kitabia. Mandhari huchangia katika kueleza mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali yao na hata husaidia katika kutambua maudhui yaliyo katika kazi za kifasihi.

Gills (1985) na Wamitila (2002) wameongea juu ya upana wa mandhari. Wanasema kuwa mandhari si mazingira tu bali hurejelea maswala mengi yakiwemo itikadi, mila, desturi, jamii na vile vile elimu. Hivyo ina maana kuwa mandhari yaweza kuhamishwa katika mazingira tofauti kulingana na muktadha. Mandhari yana elementi zake za kuyatambulisha. Elementi hizo ni kama: Eneo halisi la kijiografia, wakati katika kipindi maalum cha kihistoria kama vile msimu wa mwaka kama vile msimu wa mvua, msimu

wa krismasi, msimu wa kupanda na kadhalika au amali za wahusika pamoja na namna, desturi za maisha yao ya kila siku. Kutokana na masoni ya wataalamu tuliowataja hapo juu tumepata kuwa mandhari ni mahali na wakati ambapo matukio ya hadithi hufanyika. Tumepata kuwa mandhari husaidia kuhakiki wahusika, pia huibua hisia fulani na kutupa taswira kamili ya hali ilivyo.

Njogu na Chimerah (1999) nao wanasema kuwa mandhari ni mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbali mbali ya kazi ya kifasihi. Wanaendelea kusema kuwa mandhari ni mazingira ya wahusika pamwe na matukio, na inahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana.

Mandhari ni mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika na nafasi zao za kitabaka. Kufahamu mandhari kunatusaidia kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika. Wao wanaendelea kusema kuwa mandhari huweza kutupa mwelekeo kuhusu maudhui.

Wamitila (2003) anasema kuwa mandhari ni dhana inayotumiwa kurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia. Haya ni mazingira ya utendaji au usimulizi wake. Katika mapana, dhana hii hutumiwa kuelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa fasihi. Aghalabu wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika, lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia. Mandhari yaweza kuhusisha mahali mbalimbali kama vile nyumbani, gerezani, barazani, chumba cha ufuo, msituni, pangoni kotini na kadhalika. Mazingira nayo yanaweza kuwa ya kisiasa, kidini, kimapenzi na kimapenduzi.

Kulingana na Wamitila (2002) mandhari huwa kama kipengele cha kidhibiti cha wahusika na mazingira kama majaliwa. Yaani maelezo ya msanii kuhusu mahali fulani katika kazi yake yanaweza kutuonyesha mwelekeo maalum wa hadithi.

Wamitila (2008:303) akimnukuu Simpson katika *Stylistics* 35, anabainisha miktadha mitatu mikuu kuhusiana na mazungumzo. Muktadha wa kiakili, muktadha wa kimaumbile ambao unarejelea mandhari halisi ambapo mtagusano baina ya wahusika unafanyika. Mandhari hayo ni kama hotelini, nyumbani, gerezani au njiani. Muktadha huu hujenga nguzo za mazungumzo ya ana kwa ana baina ya wahusika. Tamthilia yaweza kuwa na muktadha mmoja wa kimaumbile au kadhaa, muktadha kibinafsi na jamii au baina ya wahusika na mazumngumuzo. Unaweza kuwa wa kijamii baina ya mtu na mkewe, mtoto na wazazi au ndugu na ndugu n.k.

Muktadha wa kiakili ni muktadha unaorejelea maarifa walio nao wahusika katika mazumgumzo. Maarifa waliyonayo wahusika yanaathiri mazungumuzo yao kwa kiasi kikubwa.

K.W Wamitila (2004) anaeleza kuwa mandhari ni sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili pia huweza kutumiwa kwa mapana kuelezea mazingira ya kisaikolojia ya tendo fulani. Mandhari huweza kurejelea yale mazingira ya jukwaani na hata wakati wenyewe. Aliendelea kutueleza kuwa kuna baadhi ya vipengele muhimu vya mandhari katika uchambuzi wa tamthilia, navyo ni pamoja na; sifa za jukwaa, eneo la uigizaji na uangazaji wa jukwaa.

### 2.4.1 SIFA ZA JUKWAA

Maleba yanayotumiwa na wahusika wa kazi za kifasihi yana mchango mkubwa kwenye athari ya tamthilia nzima. Maleba haya huweza kuakisi kipindi cha historia pamoja na hali iliyokizunguka kipindi hicho. Uteuzi wa maleba hudhibitiwa na nia ya kutaka kuizuia athari fulani. Maleba pamoja na mafigu au vinyago vya wahusika huweza kutumiwa kuwapa sifa ambazo sio za binadamu wa kawaida.

### 2.4.2 ENEO LA UIGIZAJI

Tamthiliha huigiziwa katika sehemu fulani. Hapa kuna jukwaa ambako wahusika wanaingiliana katika uigizaji wao. Ukubwa au upana wa eneo hili ni muhimu sio tu kwa athari bali pia kwa kuupitisha ujumbe fulani.

### 2.4.3 UANGAZAJI WA JUKWAA

Matumizi ya taa ni muhimu katika uigizaji. Taa hutumiwa kulimulika eneo walipo wahusika, wanaotenda tendo fulani. Taa hizi huweza kutumiwa kwa namna ambayo inazua picha fulani kuifungamanisha na tendo kuu, kwa mfano, taa nyekundu kuonyesha hatari, giza kuonyesha uovu au ukosefu wa mwelekeo.

Wamitila (2008) anasema kuwa wahusika hupatikana katika muktadha maalum. Muktadha huu si tu wa kijiografia, khiistoria, kijamii, kitamaduni au kisiasa bali pia ni mktadha wa kiisimu au kilugha. Anaendelea kusema kuwa lugha wanaotumia wahusika wa kifasihi haziwabainishi tu kama wahusika mahususi, bali pia hutambulishwa au hubainisha sajili inayohusishwa na wahusika wanaopatikana katika mazingira fulani

maalum. Wahusika wasomi kwa mfano wanatarajiwa kuonyesha matumizi ya lugha inayohusishwa na wasomi.

## 2.5 LUGHA

TUKI (1990) inasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti ambazo hutumiwa na watu wa jamii moja walio na utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Hii inashabiana na maoni ya Wamitila (2003) kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani na wenye utamaduni unaofanana kwa madhumuni ya kuwasiliana. Maana tunayopata ni kuwa lengo kuu la lugha ni kuwasiliana. Wamitila anaendelea kusema kuwa lugha yaweza kuwa ya mazungumzo, maandishi au ishara. Hivyo msanii yeyote ana uhuru wa kutumia lugha anavyopenda.

Syambo na Mazuri (1992) wanatanguliza kitabu chao kwa kusema kuwa mwandishi mzuri wa fasihi ni yule anayetumia lugha kwa njia ya kumgusa msomaji. Wanaendelea kusema kuwa msanii huyu hatumii lugha ya kawaida katika usanii wake.

Msokile (1993) naye anasema kuwa lugha ni uteuzi wa maneno yanayozingatia tamathali za usemi na ya methali.

Mgullu (1999) akimnukuu Sapir (1921) anasema kuwa lugha ni mfumo ambao mwanadamu hujifunza ili atumie kuwasilisha mawazo, maoni na maono yake.

Cook (1969) kwa mujibu wa Habwe na Karanja anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti, nasibu na ishara za kisarufi ambazo kwazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao.

Wamitila (2008:69) anasema kuwa lugha hutofautiana kutegemea mazingira au muktadha inakotumiwa lugha hiyo. Anaendelea kusema kuwa lugha inayopatikana katika kazi au matini za kifasihi ina uwezo wa kukiuka kwa sajili na kuibuka na mitindo ambayo ni jangamano. Katika utafiti wetu tumechunguza jinsi lugha inavyotumika kuathiri usawiri wa wahusika wa kike. Jinsi wahusika wengine wanavyotumia lugha kuwadunisha wanawake katika tamthilia za *Natala* na *Mama ee.*

### 2.5.1 USIMULIZI

Usimulizi katika drama unakuwa muhimu katika uchanganuzi wa tamthilia.

Wamitila (2003) anasema kuwa kazi zote za kifasihi lazima ziwe na matukio ambayo huwasilishwa kwa hadhira kuwa usimulizi. Usimlizi unaweza kuwa wa kufululiza matukio moja kwa moja au ule wa kurejeshi ambapo msimulizi hurejelea mambo yaliyopita. Kuna mitindo mbalimbali ya usimulizi, baadhi yao ni: Sahili ambao ni nyepesi kwa kueleweka au usimulizi wa kitendawili ambao msomaji na msikilizaji anatakiwa kutegua. Hivyo ni jukumu la msimulizi kuchagua jinsi ya kuwasilisha mawazo yake. Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza msimulizi hujenga uhusiano wa karibu mno na msomaji. Yeye huweza kueleza tajriba zake ili msomaji aweze kuona anachokiona, kusikia anachosikia na kuhisi anavyohisi.

Wamtilia anaendelea kusema kuwa si lazima msimulizi akajifunga kwenye usimulizi wa aina moja. Inawesekana mwandishi akautumia usimulizi maizi katika sehemu kubwa ya kazi kisha akaingiza usimulizi wa nafsi ya kwanza.

### 2.5.2 USIMULIZI MAIZI

Wamitila (2002) anasema kuwa usimulizi wa aina hii hufuata mkondo unaodhihirisha ufahamu wa siri na mambo yote. Msimulizi maizi huwa na sifa za kukielewa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, hadithi, mwelekeo na saikolojia ya viumbe wa hadithini. Mbinu ya usimulizi maizi hutumia nafsi ya tatu na ina sifa ya kuwa na uhalisia ukilinganishwa na mbinu zingine. Pia mwandishi ana uhuru; wa kuteua mambo yepi ya kusimulia na yepi ya kupuuza kufungamana na mambo hayo. Usimulizi kama huu una udhaifu. Wahakiki wanasema kuwa hamna binadamu ambaye ana sifa za aina hii lakini inatubidi tuseme kuwa mwandishi anatuelezea mambo anavyotaka kutuelezea kutokana na kaida na kanuni za kifasihi.

### 2.5.3 USIMULIZI WA NAFSI YA KWANZA

Usimulizi huu unatofautiana na usimulizi wa nafsi ya tatu kutokana na sifa yake ya kutoweza kuyaona yote isipokuwa usimulizi wa tendi. Msimulizi anayepatikana katika kazi hii huwa ana mkabala mmoja tu. Mwandishi anaweza kumtumia nguli wa hadithi katika usimulizi huu.

Leech na Short wanasema kisahihi kuwa usimulizi huu unajenga uhusiano wa kibinafsi kati ya msimulizi na msomaji. Wanaendelea kusema kuwa usimulizi huu unaelekea

kuathiri mipaka iliyopo kati ya ubunifu na hali halisi. Huu ndio msingi wa wasomaji na wahakiki kumhusisha mwandishi na mhusika wake katika kazi iliyosimuliwa katika nafsi ya kwanza.

Wamitila (2002) anasema kuwa umuhimu wa mazungumzo unaakisiwa na kauli inayotolewa na mhakiki maarufu Northrop Frye katika kitabu chake kiitwacho *Anatomy of Criticism*. Katika kitabu hiki Frye anasema kuwa drama ni mwigo au muharati wa mazungumzo au maongozi. Mazungumzo ni kipengele kinachokaribiana na uhalisi wa jinsi watu wanavyotumia lugha katika maisha ya kawaida. Wamitila anasema kuwa msingi wa kwanza wa kupimia kazi ya tamthilia ni uigizaji. Mazungumzo yanapaswa kuundwa kwa namna inayomruhusu muigizaji kuyaigiza na kutaabika kwa njia yoyote. Hii ndio njia ya pekee aliyonayo mwandishi kuyawasilisha mawazo yake. Mazungumzo yake lazima yawe na uwezo wa kuyawasilisha matakwa yake kwa njia yenye mnato. Anaendelea kuwa mwana-tamthilia mzuri lazima awape wahusika wake lugha zinazowatambulisha kama wahusika binafsi. Huko nyuma tuliona kuwa wahusika wana sifa mbalimbali: kijamii, kielimu, kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na kisaikolojia. Lugha zinapaswa kuonyesha ukweli huu. Wahusika huweza kupewa matumizi yao maalum ya misemo, nahau, methali, kuchanganya ndimi, matumishi ya lugha na hata msamiati. Nathrop Frye anasema kuwa maongezi yanapaswa kutokana na sauti za wahusika waliopo katika kazi maalum bali sio na sauti ya mwandishi. Anaendelea kusema kuwa lugha ya wahusika imefungamana na ngazi zao za kimaisha, mazingira yao na hata elimu yao. Kama vile tamthilia ya *Natala* ya Kathika wa Mberia inabainisha waziwazi lugha ya watoto na watu wazima. Tukichunguza lugha ya Bwanu na Alika (*watoto wa Natala*)

tunaona tofauti kubwa kati yao na watu wazima. Tofauti inatokea pale kwenye maswali wanayouliza, na hata kujirudia. (*Natala* uk 24)

Alika: Mami

Natala: Naam

Alika: Mami mimi mzuri?

Natala: Wewe ni mzuri sana.Kwa nini unaniuliza?

Alika: Mwalimu Jane alisema mimi ni mtoto mbaya.

Natala: Ulifanya nini?

Wamitilia (2008) anasema kuwa lugha ni nyenzo ya kimsingi na mhimu katika kuonyesha mtazamo katika kazi ya kifasihi. Ngazi ya lugha inaweza kuhusisha uteuzi wa maneno ya msimulizi, matumizi ya majina na sifa zinazohusiana na lugha ya msimulizi na kubainisha ni kwa jinsi gani ambavyo lugha hiyo ya msimulizi inavyoathiri lugha ya mhusika na kwa njia hii kuonyesha mtazamo wa msimulizi.

Wamitila anaendelea kusema kuwa katika uchanganuzi wa mazungumzo, kuna mbinu ya "usemaji kando". Kwa kawaida maneno yanayosemwa hayapaswi kuendelezwa na wahusika. Hata kama wanasikia, wanapaswa kujifanya kuwa hawasikii.Ikiwa kuna mhusika yeyote atakayeyaendeleza, itakuwa makosa, kwa sababu ameyatumia vibaya.

Anaendelea kusema kuwa mazungumzo mazuri ni yale ambayo yana matumizi ya ishara na jazanda nzito ambayo inaficha matini fulani. Kuna pia mbinu ya mazungumzonafsi ambayo ina majukumu kadhaa katika tamthilia, kwanza inaweza kuyamulika mawazo na

hisia za ndani za mhusika aliyehusika. Huweza kudhihirishia mivutano ya ndani kwa ndani aliyo nayo mhusika fulani. Hutumiwa kuwaendeleza wahusika wa aina fulana hasa wanafiki ambao vinginevyo ingekuwa vigumu kuwaendeleza. Muhimu zaidi ni kuendeleza msuko.

## 2.6 MTINDO

Mbatia (2001) asema kwamba mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kifasihi anavyotumia lugha kujieleza. Anaendelea kusema kuwa uchanganuzi huo unahusu mambo kama uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi na kwa jumla mtindo hujumuisha vipengele vyote vya lugha.

Holma (1936:515) anasema kwamba uchunguzi wa mtindo utaongeza upekee wa msanii, sifa za kawaida kama uteuzi, miundo ya aina ya sentensi, tamathali za usemi, wizani, takriri, mshikamano, msisitizo na mpangilio wa mawazo.

Wamitila (2003:145) anasema kuwa dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Anasema kuwa katika kuchunguza mtindo mhakiki anahusu kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu ya kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya na uakifishaji wake. Anataja kuwa kila mwandishi ana mtindo wake wa kipekee.

### 2.6.1 UTEUZI WA MSAMIATI

Wamitilia (2008) anasema kuwa msamiati hutumiwi kumanisha maneno magumu katika lugha bali ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Anaendelea kusema kuwa msamiati ni nyenzo ya kimsingi aliyo nayo mwandishi na ina nafasi na umuhimu mkubwa katika utunzi na uandishi wake. Jinsi ya kuwasilisha ujumbe, dhamira na tasnifu yake hutegemea msamiati na jinsi anavyoteua msamiati huo. Uteuzi wa msamiati huweza kumuadhiri msomaji.

### 2.6.2 TAMATHALI ZA USEMI

Kuhenga (1977) na Wamitila (2008) ndio wataalamu ambao wameshughulikia dhana hii. Wao wanakubaliana kuwa dhana hii hutumika kuelezea aina ya ukiushi wa kimakusudi katika matumizi ya lugha.

Holman (1936:203) naye anaeleza kuwa ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au wa kimuundo. Wamitila anaendelea kusema kuwa katika ukiukaji huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Anaendelea kwa kutoa mifano ya tamathali za usemi kama tashibihi zilizoelekea, chuku, sitiari, kinaya, tashihisi na mchezo ndani ya mchezo. Matumizi ya dhana hii huvutia wasomaji na kuwapa hamu ya kutaka kuendelea kusoma zaidi. Katika kazi yetu tumeangalia zile tu ambazo zinatufaa katika utafiti wetu .

#### 2.6.2.1 SITIARI

Hii ni tamathali ya ulinganishi isiotumia vilinganishi kama, “mithili ya”, “mfano wa”, ”ja”, “kama” na mengine mengi. Hulinganisha vitu viwili vyenye tabia sawa kwa njia ya moja kwa moja.

Wamitila (2008, 421) anasema kuwa uchunguzi wa sitiari huwezi kukamilika bila kuchunguza dhana tatu muhimu. Nazo ni: kilinganishi ambapo ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha, kilinganishwa ni kile kinachofananishwa, msingi na ile sifa yenyewe ya ulinganishi.

Mfano,

“Ujana ni moshi”

Katika mfano huu ujana ndio kilinganishwa ilihali moshi ni kilinganishi na ile sifa ya moshi ya kusambaa na kuisha bila kurudi ndio msingi ambao ujana unalinganishwa.

#### 2.6.2.2 TASHIHISI

Katika kazi ya kifasihi dhana hii ya tamathali za usemi ni muhimu. *Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika* inaeleza dhana hii kama mbinu ya uhuishi au uhaishaji ambapo vitu visivyo na uhai vinapewa sifa au tabia za kibinadamu.

Wamitila (2008) naye anaeleza tashihisi kama tamathali ya usemi ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinapewa sifa za uhai. Hii inamaanisha kuwa kuna ulinganisho wa mambo mawili hata ingawa si ya moja kwa moja. Hii ni aina moja ya sitiara.

### 2.6.2.3 KINAYA

Kulingana na Wamitila (2008) Kinaya ni usemi ambao kimsingi hujengwa kutokana na ukinzani unaotokea kati ya hali halisi na hali iliyopo.

Anaendelea kusema kuwa kinaya hutokea pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na maana inayohitajika katika muktadha maalum na inayokusudiwa na msemaji au mtumiaji. Haya maelezo yametolewa kutoka (Wales, Dictionary 224). Msingi huu ndio unawafanya wataalamu wengi kusema kuwa msingi wa kinaya ni ushirikiano wa siri katika mwandishi (msemaji) na msomaji (hadhira), umenukuliwa kutoka kwa (Short, Style 277) (Gibbs, Metaphor (365) inasema kuwa kinaya hujengwa kwenye msingi wa kuwepo na mgongano fulani kati ya hali halisi na matarajio. Hii inahalisi kusema kuwa kinaya si tu swala la lugha au balagha bali pia huhusisha akili au ubongo kwa kiazi kikubwa. Kinaya ni mojawapo ya mbinu ambazo tunazitumia sana katika maisha ya kila siku tunapokumbana na matatizo ya maisha. Tunaishi katika kipindi cha maisha ambacho wanafalsafa wengine wanakieleza kama kipindi cha baadausasa. Mambo ambayo yalikubaliwa kama ukweli yamebadilishwa na kugeuzwa. Kwa hivyo kipindi hiki kinaelezwa kama kipindi cha kinaya.

### 2.6.4 KWELIKINZANI

(Wales, Dictonary 282) Kwa mujibu wa Wamitila anaeleza kuwa tamathali ya kwelikinzani hutumiwa kurejelea kauli ambayo inaonekana kujipinga kijuujuu ingawa inapochunguzwa kwa makini inaonyesha ukweli fulani.

Uchunguzi wa kwelikinzani unahusisha mambo mawili: Utaambuzi wa kuwa kuna maana ya kijuujuu au maana ya ndani au ya kitamathali ambayo inatatua ukinzani uliopo kwa kuonyesha kwa nini kauli hiyo ina maana licha ya kuonyesha ukinzani katika maana ya kijuujuu. Kwelikinzani hupatikana katika semi nyingi za sanaa kama vile methali, nahau, vitendawili, msimu na michuuko.

### 2.6.4.1 TAASHIRA

Hii ni mbinu ambapo jina au neno linachukua nafasi ya jina au neno lingine linalohusishwa nalo kwa njia tofauti.

Kulingana na (Preminger & Brogan, New Princeton 783) wapo watalamu wanaoshikilia kuwa taashira hutokana na udondoshi fulani unaotokea katika muundo au kauli inayohusika.

### 2.6.4.2 CHUKU

Kulinga na Wamitilia (2003:145) chuku ni tamathali inayoelezea hali ya sifa ya kitu kuelezwa kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali ya kawaida. Kimsingi hapa kuna ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Sifa hii kwa kiasi kikubwa inahusishwa na kinaya. Wamitila anasema kuwa dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Kila mwandishi ana mtindo wake na ndio unamtambulisha. Mtindo unafaa kuelezwa kuwa ni njia au mbinu ya pekee anayotumia msanii kuwasilisha kazi yake.

## 2.7 HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza vipengele muhimu vya fani. Vipengele ambavyo tumevichunguza ni kama wahusika, mandhari, suala la lugha, tamathali za usemi, kinaya na ukwelikinzani. Katika sura ya tatu ambayo inafuata tumechunguza na kuhakiki uana na ubabedume kama mhimili mkuu wa ugandamizwaji wa wanawake. Kisha tukatoa historia fupi ya ubabedume na jinsi inavyochangia katika udunishaji na ugandamizaji wa wanawake katika jamii.

# SURA YA TATU: UBABEDUME

## 3.0 UTANGULIZI

Sura hii ndio inatuelekeza kwenye chanzo cha hali halisi inayowakumba wanawake katika tamthilia za *Natala* (2011) na *Mama ee* (2011). Utafiti huu umeshugulikia maana ya uana na ubabedume kama mihimili mikuu wa ugandamizwaji wa wanawake. Hii ina maana kuwa ubabedume hukuanza jana bali ni jambo la tangu jadi.

## 3.1 UANA

Wafula R.M na Njogu K (2007) wanasema kuwa suala la uana limeshughulikiwa na waandishi wengi kwa muda mrefu. Lakini kwa utaratibu maalumu limeanza kushughulikiwa kutoka miaka ya sabini. Kuna baadhi ya watunzi wanaofikiria kuwa mfumo wa kuumeni wa kukiendeleza kizazi cha mtu, ndio kadhia muhimu inayosabisha dhuluma zinazofanywa na wanaume dhidi ya wanawake. Watunzi wengine wamechanganua isimu kwamba lugha ni mali ya kiume ilivyoundwa kumtukuza mwanamume na kumdhalalisha mwanamke. Wanaendelea kusema kuwa maneno mengi yanayotumiwa kumzungumzia mwanamke yanayosawiri upungufu wake wa kimsingi kinyume na msamati unaotumiwa kufafanua sifa za mwanamume zinabainisha uwezo na utukufu wake.

Pia kuna wale wanaochuja suala la uana kwa kuzingatia mtazamo wa kisaikolojia. Lengo lao ni kuonyesha na kueleza sababu zinazowafanya wanaume kujitia wema na ukubwa. Mwachofi A.K (2011) anachunguza suala la uana kwa kuhakiki asasi ya

ndoa na jinsi inavyodhihirika kama mfumo wa kuumeni. Maoni yake ni kwamba misingi ya ndoa hii ni dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji wa wanawake.

## 3.2 UBABEDUME KAMA MUHIMILI MKUU WA UGANDAMIZWAJI WA WANAWAKE

Katika sura hii tumeshughulikia ubabedume kama muhimili mkuu katika ugandamizwaji wa wanawake. Kwanza tumeangalia jinsi ndoa, dini na elimu vinavyochochea kubaguliwa kwa wanawake katika jamii. Tumetoa ufafanuzi wa dhana ya ubabedume na mwisho historia fupi juu ya ubabedume ambayo imetupa mwelekeo wa kazi hii. Maoni ya wengine kuhusu ubabedume ni kama ifuatavyo:

Encyclopedia ya Philips (2002:282) inatoa maelezo kuhusu ubabedume kuwa:

Usemi unaotumika katika mapana yake kumaanisha uongozi wa akina baba au wanaume waliokomaa katika jamii.

Wamitila (2003:241) anaeleza kuwa "ubabedume ni mvumo wa jamii ambao unamtukuza mwanamume huku ukimdunisha na kumdhalalisha mwanamke.

Millet (1969:3) akimnukuu Sir. Henry Maine anasema kuwa: Mwanamume mwenye umri mkuu ana mamlaka zaidi kwa nyumba yake. Amri yake hudhihirika akiwa hai na hata anapoaga dunia. Katika familia za kale mwanamume alikuwa na mamlaka juu ya mali yake, bibi yake, watoto na watumishi wake wote Moi (2002:147) Akimnukuu Irigaray anayesema kwamba ubabedume ni nguvu ambazo haziwezi kipingwa zinazomzuia mwanamke kujitambulika katika jamii.

Kutokana na maoni na maelezo ya wataalamu hapo juu tunapata kwamba ubabedume ni jambo la jadi ambapo itikadi na imani za kijamii zinampa mwanamume nguvu za kutawala wanawake wao. Pia inabainika kwamba jambo hili limekuweko kwa muda mrefu ambapo ukijaribu kulirekebisha ni shida.

Mfumo wa ubabedume unampa mwanamume nguvu za kuitawala familia yake jinsi anavyotaka. Unampa mwanamume uwezo wa kumiliki mkewe na kumfanya mwanamke amtegemee kwa kila jambo. Mwanamume huyu anapata uwezo wa kumiliki ardhi aliyoirithi kutoka kwa wazazi. Watu wote katika familia ubadilisha majina na kuitwa jina la mwanamume. Kwanzia bibi, watoto, ardhi, nyumba, gari na vyote vilivyomo katika familia.

Mwanamke alikwama kwa mumewe na kunyenyekea kwa kila jambo. Liwe baya liwe zuri.Ilimbidi mwanamke kutii kila jambo ili asipatwe na kupigwa, kutusiwa na hata kuuwawa.

(Millet: 162) Ubabedume unamdhalalisha mwanamke kwa kupewa mtazamo hasi. Anaendelea kusema kuwa ikiwa mwanamke hana Jina Lake, mali yake, wala watoto wake, wana umuhimu wowote kweli? Kusema kweli ubabedume ni mfumo unaomdunisha mwanamke.

## 3.3 HISTORIA YA UBABEDUME

Inaeleweka kuwa mwanamume anapigania kumdunisha mwanamke kama njia ya kuendeleza utawala wake juu ya mwanamke. Kabla binadamu kuanza shughuli za ukulima, mwanamume na mwanamke walishirikiana katika vita. Mwanamke alijikaza kabisa hata ingawa hakumfikia mwanamume kupigana. Nguvu za mwanamume zilikuwa muhimu sana katika kipindi hiki. Alihitajika kupigana na wanyama nyikani ili akalete chakula nyumbani. Mwanamke naye alipigana na woga, ujauzito, uzazi na hedhi vilivyomfanya ashindwe na kubaki nyumbani kushughulikia watoto.

De Beauvoir (1972:95) anasema kuwa mwanamume aliweza kuikimu familia yake kwa matendo yake yaliyoashiria uasili wake wa kinyama. Tangu zamani binadamu amejaribu kuwa mvumbuzi. Mwanamume alitumia vijiti na rungu ili kujiendeleza kijamii. Katika shughuli za uvuvi ilimbidi mwanamume atengeneze matumbwi. Alifurahi sana mtumbwi huo ulipomsaidia kusafiri juu ya maji. Hii ilimpa motisha akaweza kuzidi kuvumbua zaidi. Hii ilimfanya mwanamume kuanza kuandaa sherehe baada ya ufanisi katika shuguli za uvuvi na usasi.

De Beauvoir ( 1972) anaendelea kusema kuwa maisha ya binadamu kutoka enzi za zamani yalikumbwa na hatari nyingi katika shughuli zake za usasi ambapo mwanamume alikabiliana na wanyama hatari. Alipofaulu, alijihisi kuwa shujaa dhidi ya hatari zilizomkumba. Ukoo wake ulimheshimu sana. Mwanamume alidhihirisha kuwa maisha ya binadamu hayapazwi kuchukuliwa kuwa ndiyo ya umuhimu , bali

binadamu anapaswa kushughulika na mambo muhimu ambayo yataileteа jamii ufanisi mkubwa. Kwa upande wake, mwanamke hakujihuzisha kwenye shughuli zenye hatari nyingi kama alivyofanya mwanamume. Wakati mwanadamu alipovumbua na kuanza kutumia vifaa kama visu katika shughuli zake , mwanamke alikazwa na shughuli za kuwalea watoto nyumbani.Hakuweza kushiriki katika uvumbuzi wowote. Mwanamume alitia bidii kutaka maisha yake ya baadaye kuwa bora zaidi. Hii ilimpa motisha kutalii ulimwengu huku mwanamke amebanwa nyumbani na shughuli za uzazi na malezi. Hivyo ilimbidi mwanamke amtegemee mwanamume kwa chakula na mahitaji mengine.

Millet (1970) anasema kuwa kudhulumiwa kwa mwanamke kunatokana na ubabedume unaomfanya mwanamke amtegemee mwanamume kiuchumi. Maoni hayo yanaungwa mkono na Bell na Offen (1949) wanaosema kuwa “wanawake wanawategemea wanaume kwa mahitaji yao yote”.

Shughuli za kilimo zilipoanza, binadamu alishirikisha watoto katika kufanya kazi ya shambani. Watoto wakafanya kazi ya kupalilia, jambo ambalo lilimfanya mwanamke kiumbe muhimu kwani yeye ndiye aliyewazaa wana hao.

Parpart na Sticher (1988:64) wanasema kuwa; “wanawake wana umuhimu katika familia kwani wanawazaa watoto ambao wanasaidia kuzalisha mali kwa kulima shambani. Ardhi iliyotumiwa kuendeleza shughuli za kilimo ilihitaji kurithiwa hivyo basi uzazi ukawa muhimu sana katika jamii kwani ardhi ilichukuliwa

kuwa mali ya ukoo na jamii iliishi maisha ya ujamaa. Umiliki huu wa ardhi ulileta mshikamano kati ya familia na ukoo. Ilimbidi mtu apate ardhi hiyo kwa kuirithi. Mwanamume alikuja kugundua kuwa mwanamke alikuwa na nguvu fulani. Kwani alizaa watoto kwa njia ya kimiujiza. Hata hivyo aliweza kuchimba ardhi akapanda mazao na yakamea vizuri. Sasa mwanamke akawa ndiye anayemiliki ardhi na watoto walirithi ardhi kutoka kwa mama. Mwanamume naye akajishughulisha na kazi ya uhunzi.

Alitengeneza vifaa hivyo kwa muundo alioupendelea na kwa mikono yake mwenyewe.

Mwanamume tena aligundua kuwa lazima atie bidii ndiposa aweze kufaulu. Alipotia bidii alimaliza kukitengeneza kifaa haraka. Akajua kugundua kuwa, kufaulu kwake hakukutegemea Mungu bali juhudi zake. Mwanamke naye alipanda mimea akangoja ikamea, akapalilia, akangoja tena hadi wakati wa mavuno. Baadaye aliwatukuza mababu zake kwa kuomba ili apate mavuno mazuri. Akagundua kuwa hakuna kitu kinachozuia kuimarika kwa vifaa vyake kwenye fuawe lakini mimea itaweza kupandwa na isimee. Kwa kutumia uvumbuzi huu mwanamume akaweza kuwazia mambo mengine katika ulimwengu. Hata hivyo hakuweza kutenganisha dhana ya Mungu na fauwe yake. Pia aligundua kuwa anaweza kuongeza rotuba kwenye mchanga ikiwa hatatumia shamba hilo kwa muda.

De Beauvoir (1972:109) anasema, kwa kuwa mwanamke hakushiriki kwenye kazi alizofanya mwanamume, mwanamume akamuona kama kiumbe ambaye si sawa naye. Hivyo akaishia kumwona kama kiumbe duni akilinganishwa na mwanamume.

Wolf na Witke (1975: 243) wanasema kuwa wanawake wanachukuliwa kuwa viumbe hasi wakilinganishwa na wanaume. Wanawake wanatakiwa kuwatii wazazi (baba) hadi wanapoolewa na waolewapo wawatii waume zao. Katika uvumbizi wake, mwanamume aligundua kuwa akitumia watumwa kufanya kazi ya shambani, kazi itafanyika vizuri na haraka na kweli ilifanyika vizuri kushinda ile mwanamke alivyokuwa akifanya. Hivyo katika jamii mwanamke akapoteza umuhimu wake wa kiuchumi. Katika jamii, mwanamume akawa anawatesa na kuwafanyiza kazi ngumu. Kadri alivyozidi kuwatesa ndivyo alivyojihisi kuwa na uwezo zaidi hivyo akawa na kiburi na baadaye alimgeukia mwanamke na kumweka katika kitengo cha watumwa. Hivyo hadhi ya mwanamke kwa mwanamume ilizidi kuzorota siku baada ya jingine.

Kukaendelea hivyo hadi mwanamume akawa anamiliki ardhi hivyo akamiliki na mwanamke pia. Alifanya hivyo wakati alipotaka wafanyikazi shambani mwake wawe miliki yake. Hivyo alimfanya mke na watoto wake kuwa miliki yake.

Wakati binadamu alipogundua sheria, mwanamume alikuwa amekita mizizi. Tena aliyegundua kuwa sheria ni mwanamume. Hivyo si ajabu kuwa wanaume hao waliweka sheria zinazowalenga na kuwadumisha wanawake.

Wananthropolojia wanadai kuwa ubabedume ulizuka kutokana na juhudi za binadamu kuzalisha mali. Vile alivyozalisha mali mengi, akawa anashikwa na kiburi cha ubinafsi. Hii ikamfanya binadamu kuwa na hamu ya kumiliki kila kitu kibinafsi.

Wavuti ya Jostor inamnukuu Hartman kuwa, ubabedume ulitokana na shughuli za uzalishaji mali. Jinsi binadamu alivyofanikiwa katika uzalishaji mali, ndivyo alivyogundua umuhimu wa kuwa mtaalamu na kuanza kumiliki mali binafsi. Kisha akaamua kuwamiliki wote waliokuwa na uwezo wa kuzalisha mali hayo.

## 3.4 NAMNA UBABEDUME HUDHIIRIKA KATIKA JAMII

Tuttle (1987) anasema kuwa ubabedume ni muundo wa kisiasa ambao umempendelea mwanamume dhidi ya wanawake. La msingi ni kuwa huu ni utawala wa baba. Ubabedume kama mfumo wa kijamii, huwanufaisha wanaume ambao hudhibiti nguvu na uwezo. Nguvu za mwili na ukakamavu hutumika ili waweze kuhifadhi hizo nafasi zao. Zamani, jamii za kimagharibi ilichukulia kwamba uwezo na utawala wa mume ulitokana na Mungu na ni kimaumbile.

Wanaume wanalaumiwa kuwa wametekeleza wajibu wao wa uongozi katika familia na kumuachia mwanamke kutekeleza kazi zote za nyumbani, na wanasema ipo haja ya kuuchukua uongozi huo tena. Ubabedume umekita mizizi katika jamii na kati ya asasi ambazo huendeleza ubabedume ni lugha na utamaduni.

Lugha hushikamana sana na utamaduni, kwa hivyo anayeimiliki lugha ataumiliki utamaduni. Lacan anasema kuwa tatizo la wanawake kujihisi wanyonge ni kukosa lugha. Lacan anaendelea kusema kuwa lugha ndio huwanyima wanawake uwezo wa fasihi ya uandishi. Anachokisema ni kuwa lugha humilikiwa na ubabedume. Wanaume ndio huchagua ni maneno yepi ni mwiko na yepi si mwiko. Wao ndio wanavipa vitu majina hata sehemu za nchi.

Kramarae (1965) anasema kuwa walio na uwezo wa kuvipa vitu majina duniani wako katika nafasi ya kuashiri ukweli.

Kumekua na jitihada kutoka kwa wafeministi kupinga lugha isimbague mwanamke. Ubabedume unadhihirika kupitia umiliki wa nguvu zote za uchumi. Baada ya kuzuka kwa viwanda kazi za ushonaji zilipelekwa huko, na mabwana ndio walikua mabepari wazalishi.

Spivak anasema kwamba mbali na wanaume kumiliki rasilmali na njia za uzalishaji, wanammiliki mwanamke pamoja na watoto anaowazaa. Ukweli ni kwamba mtoto ni wa baba ambaye hazai, ni mfano kwamba wanawake wamedhulumiwa na jamii ya ubabedume.

Millet (1990:33) asema kwamba kitamaduni, ubabedume ulimpa baba karibu umiliki wote juu ya mke, watoto pamoja na mamlaka ya kuwachapa, mauaji au na hata kuwauza.

Kwa hivyo utawala wa baba au mfumo mzima unamiliki uchumi na njia zote za uzalishaji. Uwezo huu unawapa nguvu za kutoa maamuzi yanayowapendelea wao wenyewe. Kutokana na uwezo huu, sauti yao ndio inatawala kila kitu.

Stitcher na Parpart (1998:39) wanasema kwamba wanawake wanadhulumiwa kwa njia ya moja kwa moja. Hapa na pale mazao au huduma wazizalishazo hutumiwa na tabaka la ubabedume. Pia kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kuwalea watoto, jambo ambalo ni muhimu kwa kunusurika kwa watoto. Pamoja na kuwa mazao na huduma za watoto hao zilidhibitiwa na ubabedume pale watakapokua wakubwa na kuanza kuzalisha mali.

Mwanamke anaendelea kutawaliwa na ubabedume kwa kuwekewa viwango mbalimbali vya kitamaduni. Ipo miiko mingi kuhusu chakula, maamuzi, vita na vingine. Katika jamii nyingi mwanamke hakuruhusiwa kula na wanaume (1998:247). Mwanamume akifa, mwanamke hana uwezo wa kutawaliwa na fahamu zake kuhusu kuendekeze maisha yake bila mume. Jamii ambayo inatawaliwa na ubabedume ndio huamua ni mwanamume yupi atakayemrithi na kuendeleza maisha yake. Mwanamume huyu ndiye huwa na uwezo juu ya bibi, mali, watoto na hata shamba la marehemu.

Tuanzie jambo lisilo bayana zaidi kuwa wanaume ndio wanaoamua tuwe na tabia gani au tujiwazilishe vipi. Kupitia sayansi, mavazi, sheria, tunaambiwa vile tunavyotakikana kuonekana, Kutoboa sikio au pua, kujifinika kichwa au uso, matiti makubwa, kutahiriwa, viuno vyembamba… hivi ni vyetu? Mavazi yatuachayo karibu tupu, viatu vituumizavyo, kuna chochote chetu? Tunavifanya hivi kujifurahisha na mitindo inayotengenezwa na

wanaume ambao wanadhibiti vyombo vya habari, matangazo ya biashara, majarida na viwanda vya manukato na ndio hutughilibu kudhania kwamba sisi ndio huonyesha njia ya mtindo.

## 3.5 HITIMISHO

Katika sura hii ya tatu utafiti huu umechunguza uana, ubabedume kama muhimili mkuu wa ugandamizwaji wa wanawake, historia ya ubabedume na namna ubabedume unavyodhihirika katika jamii. Uelewa wetu wa historia ya ubabedume umetuelekeza kupata ufahamu wa chanzo cha ugandamizwaji na udunishwaji wa mwanamke kwa wakati. Tumegundua kuwa chanzo cha mateso ya wanawake ni wanaume tu.

# SURA YA NNE: WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *MAMA EE*

## 4.0 USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *MAMA EE*

## 4.1 WAHUSIKA

### 4.1.1 MWAVITA

Mwanamke wa makamo ambaye ni wa miaka 25 hivi. Ameolewa na Kinaya. Yeye anafanya kazi katika kampuni moja na kuhakikisha kwamba aila yake inaendelea kuishi maisha ya kisasa. Mwavita avumilia dhuluma kutoka kwa mumewe kwa muda mrefu. Siku moja Mwavita alipigwa ngumi na Kinaya hali ambayo ilimfanya an'goke meno mbili pamoja na mimba yake kuharibika. Alilazimika kukimbilia kwao na baada ya wazazi wao kuwapatanisha Mwavita alirudi kwake kabla ya Kinaya kulipa fidia akizingizia mwanaye Juma. Hata ingawa walipatanishwa Kinaya aliendelea kumdhuru Mwavita.

Mwavita ni dadake Tenge. Wanadada hawa walishirikiana katika kuamua kujitetea kibinafsi na ikabidi kupigana kila wanapovamiwa na wanaume. Walishirikiana kumtandika Kinaya alipowatembelea kwenye nyumba yao mpya. Habari wanaotupa hapa ni kwamba wanawake wanaposhirikiana hawawezi kushindwa kukabiliana na maovu yanayofanywa juu yao na wanaume. Hata ingawa agizo la mahakama linathibitisha kwamba sheria zinazompendelea mwanamume, Mwavita hakukata tamaa. Wanashirikiana na Tenge kufikiria juu ya uundaji wa chama cha kina mama ambao

wanasisitiza kwamba chama chao hakitakuwa tasa na cha kitabaka, bali chama chao kitawajumuisha wanawake wote.

Mwavita ndiye kiwakilishi cha mtetezi wa jinsia ya kike. Japo amepata changamoto katika harakati za kumkomboa mwanamke amefaulu baada ya kushirikiana na dadake Tenge kukata minyororo inayomfunga mwanamke kutoka kwa mwanamume. Ameasi asasi ya ndoa hata ingawa alichukua muda kuvumilia. Mwavita ameasi asasi za dini ambazo zinazidisha dhuluma na mateso kwa mwanamke.

Mwavita : Sikiza bwana mdogo, Mungu kama kakubali kuwa mmoja wa wafuasi wa kanisa lake ni kukubali utumwa, kunyanyaswa kuonewa kupuuzwa na kunyonywa, sina haja na kundi lake takatifu.Umesema nikataswe komonio kwa ajili mimi ni mdhambi. Dhambi yangu kuu ni kukataa kunyonywa na kuwa tayari kukimu maisha. Sasa unaweza kumwambia huko kwa bosi wako huko juu andike kosa lingine katika kitabu cha makosa yangu---UASI. Sina haja tena na dini yako. (uk 86)

### 4.1.2 KINAYA

Kinaya ni mwanamume ambaye ana umri wa makamo wa miaka 33 hivi. Ni mumewe Mwavita. Kinaya anafanya dharau uaminifu wa Mwavita. Badala ya kushirikiana naye kuimarisha nyumba yao, alikuwa analewa, anafanya usinzi, na anamgombanisha na hata kumpiga Mwavita kila anapopata nafasi. Mwavita alipotorokea kwao, Kinaya hakubadilishi tabia yake asilani. Badala yake aliendelea kuchezea shere ndoa yake kila kuchao. Siku moja Mwavita naye aliamua kumuacha kabisa. Alipoendelea

kumfwatafwata, Mwavita na Tenge dadake walishirikiana na kumtandika sawasawa. Tena Kinaya anapoenda kwa wakwe zake, alichekwa kwa vile alikuwa amelewa na alienda huko akiwa amechelewa.

Kinaya anamfanyia Mwavita stihizai kwa kurudia kufanya makosa yaleyale aliyokataswa na wazazi wao. Pia anaifanyia asasi yote ya ndoa kinaya. Wajibu wa kuoa haumshughulishi hata kidogo. Ni mtu mdhalimu anayempiga mkewe hata wakati yeye ni mgonjwa. Anapelekwa mahakamani na mkewe kwa kosa la kumpiga ngumi na kumngoa meno mawili na pia kufanya miimba kuavya. Mahakama inampendelea Kinaya kwa kumpatia mtoto wao Juma na Mwavita kumuona kila mwezi mara mbili. Kinaya ni mhusika muhimu kwa sababu yeye ni kiwakilishi cha wanaume wengi ambao wanaamini kwamba mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume.

### 4.1.3 TENGE

Mwanamke mbichi wa umri wa miaka16 hivi. Alikuwa katika kidato cha tatu, aliponekana akilia kwa uchungu mwingi kwa sababu katiwa mimba na George. George alikataa kumpeleka kwao hadi amalize kidato cha sita. Nyumbani pia Tenge kapigwa na babake na kakake (wanaume) na kufukuzwa. Mamake mzazi ndiye aliyeungana na Tenge kupigania haki katika jamii. Wao wako pamoja kushinda udhalimu unaotekelezwa kwao na wanaume. Tenge na mamake wanalalamika kuwa hakuna haki na usawa katika jamii. George naTenge walishirikiana katika kitendo cha kuzini lakini taasis ya elimu inamruhusu George kuendelea na masomo na Tenge naye kufukuzwa shule. Tenge aliwakashifu vijana wanaume kwa ubinafsi na unafiki ambapo wao ndio wanawanajisi

wanawake halafu baadaye kuanza kuwakashifu. Wao wanashiriki nje usherati na kuwapachika mimba hao kina dada halafu wanaanza kuwakashifu.

Tenge daima humuhimiza dadake kupigania haki yake kwa ukcha na upanga. Alishirikiana na dadake kumwadhibu Kinaya alipokuja nyumbani na fujo.

### 4.1.4 MAMA

Mama yake Mwavita na Tenge na ni mkewe Mzee Tembo. Anaungana na Tenge kupigania haki katika jamii. Wako pamoja kushinda udhalimu unaotekelezwa kwao na wanaume. Wakati Tenge anafukuzwa shule, anakoenda anatarajia mateso mengine kutoka kwa wanaume (babake na kakake) ambao si tofauti na George. Mwokozi wake Tenge ni mamake ambaye pia anaelekea kuadhibiwa kwa sababu ya bintiye ambaye amepachikwa mimba na George. Kulingana na wanaume, makosa ni ya wanawake wote. Mama amewahimiza wanawake wenzake kutia bidii na kuungana kutetea haki za wanawake wenzao katika jamii iliyotawaliwa na ubabedume.

Mama ana matatizo kwa sababu bintiye (Mwavita) amepigwa na kuumizwa na mumewe. Tenge naye ni mjamzito. Licha ya Mwavita kumwonyesha Tenge mfano bora, anaharibiwa na George. Ingawa Tenge naye amekosa, mama anamhakikishia kuwa ni bintiye daima. Hii inaonyesha umoja walio nao wanawake. Pia anamkataza Mwavita kutorudi kwa Kinaya tena kwa sababu Kinaya amewaua watoto wake wawili katika vita vyake naye kila mara apatapo nafasi. Mama Alimwambia kuwa wake (Mwavita) naye akifa, naye atakufa kwa sababu hawezi kustahimili mateso wanayoyapitia wanawake.

### 4.1.5 PADRE

Ni Mwanamume ambaye anaaminika kuhubiri neno la Mungu. Anatumiwa na Kinaya kumshawishi Mwavita (mkewe) ili arudi kwake hata ingwa anajua kuwa Kinaya ndiye aliye na makosa. Padre ni mwanamume ambaye haoni kosa lolote linalomfanya Mwavita kumuacha mumewe.

Padre: "… mwanawe mama nimesema naye mara nyingi bila kufaulu. Ni mkaidi kama Wayahudi walivyokuwa waliposemeshwa na kuonywa na manabii hapo kale. Tangu alipokuwa mgonjwa sana hospitalini nilimwambia kuwa, kwa vile walioana kanisani, lazima amsamehe mumewe. Ndoa ni sakramenti kubwa ya kanisa la Mungu hapa duniani."

Padre anasema kuwa watu wakioana kanisani huwa mwili mmoja na roho moja. Hivyo siku ile walipofunga ndoa katika kanisa la Mungu walifunganishwa wakawa hivyo. Ameongea juu ya Mwavita kuwa hospitalini akiwa mgonjwa sana kwa ajili ya kupigwa na Kinaya. Yeye amechukulia kuwa mwanamume ana haki ya kufanyia mwili wake vile anavyotaka. Anasema kuwa Mwavita hana madaraka kujitenganisha na mumewe. Kwake Padre, Mwavita anavunja sheria za Mungu. Anastahili kuendelea kukaa na mume ambaye ni muuaji kwa ajili ya kuchunga sheria za Mungu ambazo zinamdhalalisha mwanamke.

Padre ni mtu ambaye anataka kuwa, akisema na Mwavita asiulizwe swali. Kwa vile yeye ni mtu wa Mungu na ni mwanamume anastahili ile heshima kutoka kwa mwanamke.

Padre: (*akimwambia mama*) Unaona mama! Ndivyo asemavyo siku zote haishi maswali na mambo mengi ya kuhalalisha kitendo chake kiovu cha kuivunja ndoa ya Mungu.

Padre anajua kuwa yule anayetoroka ndoa yake ndiye mhalifu. Anayeenda kinyume ya ndoa na kufanya usherati pamoja na kumpiga mkewe, ana haki ya kufanya hivyo. Hivi ndivyo asasi ya ndoa na dini zinavyombagua mwanamke dhidi ya mwanamume.

Mama: Lakini Padre, huoni kuwa Kinaya aweza kumuua.Wewe ulimwona hospitali vile hali yake ilivyokuwa. Hujui kuharibu mimba ni kifo?

Padre: Lakini Kinaya amejuta na kunijia mimi na kuniomba niseme na mkewe.

Padre hata akikumbushwa hali ya Mwavita baada ya kupata mateso kutoka kwa Kinaya bado anamtetea mwanamume (Kinaya). Kwake Padre, Kinaya ni mwanamume ambaye ana haki ya kusamehewa hata ingawa ameua mara mbili. Na kuwa mtu wa Mungu, infaa Mwavita askize na kutenda vilivyo. Huu ni ubabedume unaodhhirishwa na mtu wa Mungu. Padre anathibitisha vile asasi ya dini inavyombagua mwanamke.Padre hataki kusikia sauti ya mwanamke. Hata Tenge anapojaribu kuongea kwa kuuliza maswali, kwake yeye hayo ni matusi kwa kazi ya Mungu. Padre ni mwanamume hata ingawa ni mtumishi wa Mungu, ambaye hamjali mwanamke kama binadamu mwingine. Akitumia sheria za Mungu amtaka mwanamke kujinyenyekea mbele ya mwanamume. Yeye hajaoa

kwa hivyo hajui kumtunza mke, kuna maana gani. Hana ujuzi juu ya yanayojili katika familia. Anataka mwanamke atunze sheria na kumpa mwanamume kushika ushukani akiwa kwake. Ni mtu anayeonyesha dharau kwa mwanamke kama vile, wakati Tenge anamuuliza maswali, anaona kuwa hayo ni matusi kwa kazi ya Mungu na kuwa anamkumbusha ana dhambi ambayo hajatubu.

Padre: "(*kwa hasira*) unatukana kazi ya Mungu. We nyamaza. Huyo mwanao hajabatizwa na hatabatizwa kwa ajili ya kosa lako wewe. Usikufuru ukajipalia makaa ya moto."

Padre anaona kosa la Tenge la kupata mtoto ni lake na hata litamzuia kujiunga na kundi la Mungu kwa kutobatizwa. Yeye hana heshima maadam ni mwanamke. Anamfokea Tenge kwa kumnyamazisha "we nyamaza".Anamwona kama mtu asiye na haki ya kuzungumza mbele ya mwanamume. Padre ni mwanamume ambaye hajaoa lakini anauendeleza ubabedume. Hii ni dhibitisho jinsi dini inavyondunisha mwanamke.

### 4.1.6 WANAKIJIJI

Wanakijiji ni wazee wanaotoka mahali ambapo Mwavita na Kinaya walikozaliwa na kulelewa. Wanakiji hawa wakiongozwa na mzee wa kizamani ambaye hamthamini mwanamke. Kinaya aliposhtakiwa kwa wanakijiji na Mwavita, wanatoa adhabu ambayo haitoshi kufidia makosa ya Kinaya. Kinaya aliharibu mimba ya mkewe mara mbili ambayo ni makosa ya kuua na kumn'goa. Mzee wa kijiji anakiri kuwa adhabu aliyowekewa haitoshi kufidia makosa ya Kinaya. Ba mkubwa wa Kinaya akaikubali mara moja kuwa inatosha. Hata baada ya kukubali kufidia kosa lake kwa vichache alivyoulizwa, Kinaya anamtaka mkewe arudi hata bila yeye kulipia adhabu yake.

Mkutano ulipokwisha Mzee wa kijiji na wazee wengine walimwita nyanya na kumwarifu kuwa waende wakamfunze Mwavita jinsi ya kuishi na bwanake. Wasiketi naye bure wakimwangalia akienda mrama na wao hawamwambii. Mtazamo huu basi unatuarifu kuwa wanawake ndio wamekosea kuwapa mabinti zao mawaidha kabla ya kuolewa.Mzee wa kijiji ambaye ni jaji mkuu wa kesi ya Kinaya na Mwavita ana mtazamo kuwa mwanamke anapaswa kukubali yote anayoambiwa na bwanake bila kuuliza maswali. Anaeleza kuwa zamani, mwanamke akikataa kumrudia bwanake baada ya kukosana alikuwa akilazimishwa. Hiyo lazima, ilikuwa kwa kufungwa kidole kwa uzi mwembamba usioweza kukatika haraka. Uzi huo hukazwa sana na huvutwa na kufungwa kwenye nguzo ya nyumba. Wazee basi humuuliza kama atarudi au sivyo. Akikataa hukazwa zaidi hadi akubali kurudi.

Jamii hii pana inashikilia kuwa mwanamke hapaswi kuwa mbali na mwanawe. Kila mara Mwavita anakumbushwa kuhusu mwanawe. Kinaya asema kuwa bado yuampenda mkewe. Amtaka arudi hata kama Mwavita hamfikirii yeye amfikirie mtoto wao. Mama Kinaya amwambia Mwavita kuwa akaze moyo mambo yaishe ili aweze kuishi na mwanawe. Nyanya naye asema kuwa hakuna mama anayeweza kumwacha mwanaye bila sababu nzuri yenye maana. Mjombake Mwavita naye anafikiria kuwa mke akishatolewa mahari na kuolewa, basi ni mali ya yule aliyemwoa. Alimuuliza Mwavita kwa nini anamwonyesha Kinaya (mumewe) ujeuri.

Wanakijiji wanamwekea mwanamke lawama kwa kila jambo na hawaoni sababu ya Mwavita kumwacha mumewe na mtoto. Kama nyanyake Mwavita ambaye ni kiwakilishi

cha enzi ya zamani anamwambia Mwavita kuwa mwanamke sharti amtumikie mumewe kwa kila njia. Kuwa ni lazima ampikie mumewe hata kama ni saa sita ya usiku. Hii ndiyo kazi yake hata mumewe akija akiwa mlevi asimwonyeshe tabia yeyote ile. Hii ndio inaonyesha jinsi utamaduni unavyomdhalalisha mwananamke.

## 4.2 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA TAMTHILIA YA *MAMA EE*

K.W .Wamitila (2008:295) asema kuwa matumizi ya lugha katika tamthilia huwa ni kupitia mazungumzo. Nayo mazungumzo huweza kutofautishwa kwa njia mbili kuu. Njia ya kwanza ni mazungumzo ya moja kwa moja baina ya wahusika na pili mazungumzo ya mdokezo ambayo huwa ni baina ya mwandishi na msomaji au msimulizi na mhusika.

### 4.2.1 UZUNGUMZINAFSI

Katika kipengele hiki utafiti huu umechunguza jinsi wahusika wanavyotumia lugha wakati wanamlenga mhusika wa kike. Katika onyesho la kwanza Mwavita anajizungumzia anaposikia mlio wa gari. Mazungumzo yake yanaasheria mateso aliyonayo ambayo yanaletwa na Kinaya mumewe. Kinaya amemuachia kazi zote na kujitoma katika lindi la ulevi na uasherati. Hii inamfanya Mwavita kutumia maneno kama, laja, ni kama nilifiwa, sina wakunisaidia, jiume, lenyewe, levi, lazurura na mgogo wa gari likibadilisha wasichana kama mashati, leo nalipigia simu mara nne bila kufaulu.

Uzungumzi nafsi huu wadhihirisha ile hasira aliyokuwa nayo Mwavita kwa mumewe. Kinaya anapofika mlangoni anatumia lugha ya madharau kwa mkewe. Hii yaonyesha kuwa ni wajibu wa mwanamke kukaa na kungoja mumewe na kufungua mlango mara tu mumewe afikapo. Kinaya hamtambui Mwavita kama mtu wa maana anapomwita 'mwanamke'.

Uzungumzinafsi pia umetumiwa na Tenge katika onyesho la pili. Naye analia kuwa Mwalimu Mkuu kamfukuza shule kwa sababu ana mimba. George naye kakataa kumpeleka nyumbani kwao eti asema amalize kidato cha sita kwanza ndipo amsaidie. Anashindwa la kumwambia mama na anasema kuwa mamake atakufa. Analia kwa kumtaja mama kuwa yeye hataweza kumsamehe. Hii inaasheria taabu aliyonayo Tenge msichana mbichi wa kidato cha tatu ambaye amepachikwa miimba na George kijana wa kidato cha sita.George amwambia kuwa lazima amalize shule kwanza ndiposa aje kumsaidia. Kauli hii yaonyesha woga alionao mwanamke kwa mwanamume.

Tenge: Babangu ataniua. Mamangu atakufa. Nitawambia nini? (uk 11)

Kuonyesha kuwa kosa la mwanamke mmoja ni kosa la wanawake wote. Kulingana na mwanamume yeye ndiye aliye na mamlaka kwa nyumba yake.

Kinaya: "Mimi ni mume wako na ndiye mwenye amri katika nyumba hii yangu Usifikirie hiyo elimu yako na kazi ya mshahara imekufanya mume sawa na mimi…" (uk 3) Hii inaonyesha kuwa mume anapomuoa mwanamke, anammiliki na yeye ndiye huwa na amri bila yeyote kusema kitu. Hata ingawa Mwavita ana elimu na anafanya kazi, hadhi hiyo yote inashushwa na mumewe kwa kuolewa na kulipiwa mahari.

Kinaya: "...baba zenu siku hizi wanawauza. Mimi nililipa shillingi elfu mbili zaidi kwa kuwa ulifika kidato cha sita. Wengine hulipa zaidi, sikununua nini?" (uk 5)

Maneno haya ya Kinaya ni ya kumdhalalisha mwanamke. Kuwa wanaume hulazimishwa kutoa mahari nyingi kwa wanawake waliosoma. Hivyo hiyo mahari ni ya kuwanunua.

Mwavita: "......Usifikirie kuwa tabia yako ya uasherati kila mtu anayo. We zurura na kila jike lililo hapa mjini mradi tu usifanye tena mara ya pili kosa la kuniambukiza magonjwa yako....."(uk 6). Kinaya ni mtu anayefanya uasherati na mahawara wa mjini hata amewahi kumuambukiza magonjwa mkewe. Kinaya hana heshima ya taasisi ya ndoa. Anamwambia bibi yake kuwa huo ugonjwa umekua wimbo kwa hivyo anaweza kusimama juu ya K.I.C.C. na kuwaimbia watu. Hii ni njia moja ya kumkanya Mwavita asiendelee kumtangaza kuwa alimwambukiza ugonjwa. Kwa wanaume mambo yao hayatangazwi. (uk 7)

### 4.2.2 MAZUNGUMZO BAINA YA WAHUSIKA

#### 4.2.2.1 MAMA NA MWAVITA

Mama: Aweza kuja na ulimi wa sukari ukamkubali ati! Wanaume wajanja.

Mwavita: Usiwe na shaka sitarudi tena.

Mama: Ukitaka kurudi kwanza ujue kuwa Kinaya ameua watoto wawili kwa mikono yake. Nawe uliponea chupuchupu. Watoto wako walikufa ukastahimili. Mimi wangu akifa sasa nitakufa pia maana nimekonga siwezi kustahimili, umeelewa hivyo? Nimeshakuwa nyumba ya udongo isiyostahimili vishindo.

Mwavita: Ee ndiyo mama.

Mama: Ujue kuwa mume ni mnyama. Unaweza kumfuga lakini bado unyama wake upo. Ni kama yule mzee wa hadithi aliyemfuga simba. Mwisho simba huyo alimuua. Unakumbuka mke wa Hassan aliyepigwa sana na mumewe kwa kuwafuata watoto? Mamako mdogo wamkumbuka ingawa ulikuwa mdogo alipigwa akaharibu mimba ikamwua! Mifano ya unyama wa kiume ni mwingi sana, ukimrudia bwanako usirudi kwa hadaa ujue wazi unalofuata na uwe tayari kwa lolote." (Uk 80)

Hawa ni wahusika wanawake, lugha yao ni ya kumkomboa mwanamke kutoka mikononi mwa wanaume. Wanamlinganisha mwanamume na simba ambaye hana huruma. Kinaya alikuwa anampiga Mwavita na aliweza kumuavya mimba mara mbili. Hii ni kuonyesha unyama wake kwa mkewe. Maneno ya mama ni kumliwaza bintiye na kumwonya juu ya hatari ya kurudi tena kwa mumewe. Mama anampa mifano ya ndoa ambayo imeishia kuuawa kwa mwanamke iweze kumpa taswira ambayo ingemsaidia kuamua kutorudi kwa mumewe tena. Anaendelea kusema kuwa Mwavita akifa pia yeye atakufa kwa vile amelegea kama nyumba ya udongo isiyostahimili mateso. Hii inayaonyesha mapenzi ya mama kwa mwanaye msichana. Mwana akipitia shida yeyote, shida hiyo humsumbua mama hata ingawa hawako karibu.

#### 4.2.2.2 BABA, TENGE NA KAKA

Baba: (*kwa mabezo na kuiga*) "kosa la mara moja" nisikuone nyumbani kwangu tena.(*Tenge alia zaidi* ) Toweka kabisa mbele ya macho yangu na usiniite tena baba..." (uk:15)

Kaka: Ana nini mbona wampiga?

Baba: Si limepachikwa mimba na George. Niambie pesa zangu nitazipata wapi? Hilo George litamwoa jana la shule?

Kaka: (*Kwa hasira anarukia fimbo na kumpiga Tenge*) nilimkanya na hilo George lake.

Tenge: (*akifuta machozi)* wewe una nyingi kunishinda mimi. Pesa ulizopoteza hazihesabiki na huishia ukishikwashikwa na polisi… (Uk 17). Baba na kaka ni sauti ya wanaume ambao wanachukulia mwanamke kama ambaye anajiletea shida. Kiumbe duni ambacho kinadanganywa na kupachikwa miimba. Kosa la mara moja tu linawafanya wanaume kumfukuza mwanamke nyumbani. Huu ni udhalalishaji wa hali ya juu. Tenge anamkumbusha kaka kuwa hata yeye anafanya makosa kama hayo kwa kuwapachika wasichana watatu miimba. Hata yeye alisomea pesa za baba na kuachia shule njiani. Huku ni kuonyesha kuwa naye alipoteza pesa nyingi lakini yeye hajafukuzwa nyumbani. Lugha hii inaonyesha kuonewa kwa wahusika wakike. Mwanamke amebaguliwa na lugha ya hawa wanaume wawili.

Wakati huu Tenge anapopata shida George yeye anaendelea na masomo. Ubaguzi kwaTenge ambaye ni mwanamke. Hii inaonyesha kuwa ni kawaida wanaume kuwaharibu wasichana wadogo na kutoonekana na makosa bali makosa yanabaki kwa msichana ambaye anapitia mateso makubwa. Mateso hayo ni kama kuchapwa, kufukuzwa shule, kufukuzwa nyumbani pamoja na kuitwa majina mabayamabaya.

## 4.3 MANDHARI YA TAMTHILIA YA MAMA *EE*

Mandhari ni wakati au mahali pa utokeaji wa tukio au matukio katika kazi ya kifasihi. Muktadha wa mandhari waweza kuwa wa, kiakili, kimaumbile, kibinafsi au wa kijamii.

### 4.3.1 MANDHARI YA USIMULIZI

Kama tulivyokwisha kuelezea ni kuwa mandhari ni mahali au wakati tukio au matukio ya kifasihi hutokea. Mandhari mhusika anamojikuta huweza kuwa nguzo muhimu kwa kutia motisha matendo ya wahusika.

K.W. Wamitila (2008:351) Anasema kuwa dhana ya mandhari huweza kueleza mazingira ya kijamii na kielimu wanamojikuta wahusika wa kifasihi. Wamitila anaeleza kuwa kuna elementi zinazounda mandhari, nazo ni tofauti kabisa. Kuna mahali halisi ya kijiografia, kuna shughuli za wahusika na hali yao ya maisha ya kila siku. Kuna wakati wa kupindi maalumu cha kihistoria na mandhari pia hujengwa kwa mazingira ya kijumla ya wahusika.

Katika kazi yetu tumeangalia vile mandhari yanayohusishwa katika tamthilia ya *Mama ee* yanavyowasawiri wahusika wa kike.

Mwandishi anatanguliza kwa mandhari ya sauti ya mtoto aliaye na msichana anamuongoa kwa wimbo. Kisha fujo na mayowe ya wanawake wanaomboleza kwa kelele sana na kwa sauti ya kusikitisha sana. Wanawake watatu wanapanda jukwaani polepole. Wawili wanapiga mayowe na kulia kwa kwikwi. Mmoja wao akisikitika sana maana ni mtoto mbichi wa miaka 16 hivi, ana miimba na amevaa matambara, ameweka mikono kichwani akilia. Wa pili ana mtoto mchanga mkononi aliyefunikwa vizuri. Mama huyu amevaa vizuri lakini pia analia kwa uchungu mwingi. Wa tatu anayepanda jukwaani ana mtoto mgongoni, kitunga kikuukuu alichokiangika begani na tita la kuni

kichwani. Amelemezwa sana na mizigo hiyo. Yeye halii lakini anaonyesha huzuni na ananung'unika. Mara kwa mara anawatazama hao wawili waliao wakipunguza mayowe, asema huku akitua tita la kuni na kitunga."(uk i-v).

Mandhari haya yanawajumuisha wanawake wote, kumpa msomaji picha kuwa haya ni maswala ya wanawake na kuwa wanawake wa hali zote za maisha wana matatizo. Msichana wa miaka kumi na sita ambaye ana mimba ni kiwakilishi cha wasichana vijana ambao wanadanganyika na wanaume vijana na kutiwa miimba kabla ya kumaliza shule ilhali vijana wavulana wanaendelea na masomo yao. Mwanamke wa pili ni mama aliyevaaa vizuri na ni mama anayewakilisha kina mama wa mjini. Na wa tatu ni mwanamke anayewakilisha wanawake wa mashambani. Mandhari haya ya utangulizi yanawajumuisha wanawake wote katika jamii ilimradi ni mwanamke ana shida. Haijalishi mazingira anamoishi au umri wake, tabaka anamojikuta au hata akiwa anafanya kazi au hafanyi, yeye ana shida zake mahususi.

Onyesho la kwanza, mandhari yanayojitokeza ni usiku sebuleni kwa bwana Kinaya. Kwasikika mlio wa gari kwa mbali. Aingia Mwavita, ni mama wa miaka 25 hivi na amevaa nguo ya kulala na kujifunga leso vizuri. Anaonekana kuwa mchovu sana pia mwenye ghadhabu maana kununa sana. Sebule ni ya kisasa, ina kila aina ya chombo cha starehe – redio, T.V, kinanda na kadhalika. Viti pia ni vya starehe na taa ya rangi ya manjano anaiwasha Mwavita.(uk 1)

Mandhari haya yanawajumuisha wanawake wa mjini na wale wanaofanya kazi. Mazingira haya yana sebule ile ambayo mtu anayeishi mjini anafaa kuwa nayo. Sebule ambayo ina vitu vya starehe na vile vya watu ambao wanapata mshahara kila mwezi. Kuna kampuni anapofanya kazi Mwavita ambapo Kinaya anataka Mwavita asimamishwe. Kuna pia kampuni anapofanya kazi Kinaya. Kuna kuzurura kwa Kinaya na kila jike la mjini na kuambukiza magonjwa. Kuna kuwa na gari la kuendea kazini.

Mwavita hata ingawa wana gari, nyumba nzuri, wote wanapata mshahara na wamepata mtoto Juma, mandhari yanayojitokeza ni haya: "anampiga ngumi mdomoni na kumwacha chini. Mwavita apiga kelele na kujaribu kukimbia lakini Kinaya amshika. Wanamenyana wote na kuanguka chini. Waendelea kupiga kelele wakati ambapo Mwavita atema mate yenye damu na kulia sana kwa uchungu. Majirani wabisha kuuliza kuna nini.......... Fujo yaendelea kwa muda. (uk 10)

Mandhari haya yaonyesha kuwa hata ingawa mwanamke anaishi kwenye mazingira yasiyohitaji chochote, ilmradi yeye ni mwanamke ana shida zake mahususi.

Katika onyesho la pili mandhari ni ya mashambani ambapo tunamuona Tenge yuko njiani karibu na nyumbani kwao aliyebeba sanduku. Atembea polepole huku akilia kwa kwikwi, anapofika karibu na nyumba analitua sanduku na kuzidi kulia na kuomboleza. Ni msichana wa shule wa miaka 16. (Uk 11) Mwalimu mkuu kamfukuza shule kuwa kapachikwa miimba.

Haya ni mazingira ya shuleni ambayo yanawatenga watoto wasichana na wanapopachikwa mimba na watoto wavulana. Tenge amefika katika kidato cha tatu ilhali George aliyempachika miimba yuko katika kidato cha sita. Mazingira haya yanamkabili George (mvulana) kuendelea na masomo yake, na kumtenga Tenge ambaye ni mwanamke.

Tenge anamlilia mamake amsamehe na baba anaposikia anatamka kuwa "ondoa aibu hii kijijini mwangu" na anaanza kumwadhibu. Kakake Tenge naye anapoona hivyo anajiunga na baba kumchapaTenge. Mama tu ndiye anajaribu kumjali Tenge na hali aliyonayo. Mandhari yanambagua mtoto mhusika wa kike.

Katika onyesho la tatu ni wakati wa magharibi na mandhari ni nje ya nyumba ya mzee Tembo babake Mwavita. Wazee wameketi kivulini wamejipanga kwa msitari unaofanya thuluthi mbili za duara, upande mmoja wameketi jamaa yaani babake, mjombake, babamkubwa, nyanyake na mamake. Upande wa pili wameketi jamaa zake Kinaya, yaani babake Kinaya, babake mkubwa, kakake Kinaya, mamake na Kinaya mwenyewe. (uk 22)

Mandhari haya yanaonyesha katika upande wa Mwavita, kuna wanaume watatu na wanawake wawili na upande wa Kinaya kuna mwanamke mmoja na wanaume watatu. Pia kuna mzee wa kijiji ambaye amesimamia mashtaka. Mazingira yanawabagua wahusika wanawake kwa idadi ya mashtaka. Mwavita ndiye amemshtaki Kinaya kwa kumpiga na kuharibu miimba na pia kumwachia majukumu yote ya nyumbani.

Kwa upande wa waliohudhuria mandhari yanambagua mhusika wa kike kwa idadi. Kama vile kwa upande Mwavita waliohudhuria walikuwa wanawake wawili ma wanaume watatu na upande wa Kinaya waliohudhuria ni wanaume wanne na mwanamke mmoja.Idadi ya wanaume waliohudhuria ilikuwa nyingi kuliko idadi ya wanaumme. Hii ni thibitisho vile mandhari haya yanavyombagua mwanamke.

Onyesho la nne ni baada ya mwaka mmoja na mahali ni sebuleni kwa Kinaya siku ya Jumamosi. Mwavita aonekana mjamzito ambaye aonekana mnyonge maana ameketi kwenye sofa akijishika kichwa na kuugumia. Tenge aingia akiwa na wasiwasi juu ya hali ya dadake. (uk 59)

Mwavita alirudi kwake hata kabla ya Kinaya kulipa fidia aliotozwa na wazee kwa kuzingizia mtoto wake Juma. Anapoingia Kinaya akiwa amelewa na nguo zake chafu, nywele hazikuchanwa ayumbayumba kidogo lakini ajaribu sana kuwa wima. Kinaya amtaka Mwavita waende kwenye sherehe bila kumjulia hali yake.

Kinaya: nitapata mwingine huko shereheni na nikirudi usinipigie kelele. Kaa hapa na "naummwa" yako.Wake wenzako wana miimba na nawaona shereheni. Wewe "naumwa" "naumwa" siku zote, shauri yako. (Atoka) (uk 65)

Kinaya anapotaka kuondoka, apata nguo zake hazijapigwa pasi. Hasira zampanda na kuanza kutukana Tenge kuwa alikuwa anafanya nini ikiwa dadake alikuwa mgonjwa, na Mwavita anapojaribu kumkanya, Mwavita apigwa kofi usoni linalomwangusha. Ashika

kichwa kwa maumivu kisha Kinaya aanza kumfukuza Tenge. Badala yake Mwavita na Tenge wanatoka na kumuachia nyumba yake. Mazingira haya yanawabagua wahusika wanawake kwani Kinaya hataki kujua hali ya Mwavita (mwanamke). Yeye anataka mambo yake yatendeke vile anavyotaka. Pia mandhari yanaonyesha umoja walionao wana dada hawa wawili. Walipotoka kwa Kinaya walienda wakakodisha nyumba ambayo waliipamba kuliko ile ya Kinaya. Hapa hata wakaweka mziki wa taratibu. Mama aingia na kuwaliwaza kisha baadaye Padre akaja. Padre ataka Mwavita amsamehe Kinaya na warudiane kwa vile maandiko yasema kuwa (matt, 19.6) "kwa hivyo hao si wawili tena bali ni mwili mmoja. Kwa hivyo chochote Mungu alichokiunganisha mwana-adamu yeyote asitenganishe."

Mandhari yanawabagua wahusika wa kike kwa sababu Mwavita ndiye anayestahili kumsamehe Kinaya baada ya kumng'oa meno mawili na kuharibu mimba mbili. Pia yanaonyesha ule umoja wa wanadada hawa wa hali na mali.

Katika onyesho la pili ni mandhari ya mahakamani mchana. Kesi iliyoletwa hapa ni ya Mwavita na Kinaya na ni ya talaka na atakayeishi na mtoto. Talaka inatolewa na mtoto kupewa Kinaya kuishi naye. Mwavita amewekewa masharti kuwa atamuona mwanaye mara mbili kila mwezi. Kinaya haruhusiwi kwenda kwa Mwavita kuepuka ghasia na zogo, na katika kesi kila mmoja atajilipia.(uk 96) Mandhari haya yanambagua Mwavita kwa kumnyima mwana kuishi naye na vile mtoto ni mdogo ambaye anahitaji malezi ya mama.

Onyesho la tatu baada ya miaka kadhaa ni sebuleni mwa Mwavita ambako kunaonekana nadhifu na starehe zaidi. Wanadada hawa wawili wanazungumza kuhusu George aliyempachika Tenge mimba na kumuacha.(uk 111). Mandhari haya yana utulivu mwingi na furaha baada ya wanawake hawa kukata pingu za utumwa na kuachana na ndoa ya machozi ya Kinaya. Juhudi za Kinaya kurejesha ndoa yake kwa kutumia Padre hazikufua dafu hadi aliamua kujileta mwenyewe. Wote hao wanaishia kumuaibisha Kinaya hasa wakati wanamchapa na kumuumiza na hata kumvua nguo zake. Huu unaonyesha ushindi wa muungano wa wanawake na ni mandhari yanayoonyesha mwanamke akijitawala kumfanya Kinaya kunyenyekea kwa Mwavita. Kuungana kwa Mwavita na Tenge kwaleta ushindi katika vita vya ukombozi wa wanawake.

Mandhari ya mwisho katika chama cha umoja wa kina mama. Viongozi wa chama cha wanawake ni wanawake waliosoma na wenye madaraka ya juu na wa tabaka la juu. Hawa ni wale ambao hawajui kabisa taabu wanazozipitia wanawake wa tabaka la chini. Taabu kama kutembea masafa marefu kutafuta kuni au hata maji. Wao wameletwa na mabwana zao kwa magari makubwamakubwa. Mandhari haya nayo yanawabagua wanawake wa tabaka la chini.

Mwavita na Tenge wana nia ya kuwaunganisha wanawake wote. Wao wakiwa wa mjini wajiunge na wanawake wa mashambani ili kupata nguvu nyingi za kurekebisha asasi ambazo zinawadhulumu wanawake ambazo ni ndoa, utamaduni na dini.

### 4.3.2 HITIMISHO

Katika sura hii ya nne utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Mama ee (2011)* ambapo ulihakiki, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha na jinsi vipengele hivyo vya fani vinavyomsawiri mhusika wa kike katika tamthilia hiyo.Umeonyesha kuwa mandhari katika tamthilia ya *Mama ee* (2011) yanambagua mwanamke lakini tukapata kuwa wanawake wakiungana pamoja watashinda vita vya ukombozi wa wanawake.Utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu umejenge maudhui ya jinsi wahusika wa kike wamesawiriwa katika kazi hizi mbili.

# SURA YA TANO: WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA*

## 5.0 USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA*

## 5.1 MANDHARI YA TAMTHILIA YA *NATALA*

Onyesho la kwanza latuonyesha mandhari ya sebuleni mwa Natala na Tango Mwina ambako kuna milango mine. Kuna mlango wa kuingia chumba cha kulala cha Tango na mkewe, mlango wa kuingia chumba cha watoto, kuna mlango wa kutoka nje na pia kuna ule wa kuingia jikoni. Ndani kuna kabati limeegemezwa pembeni baina ya mlango na chumba cha wazazi. Pia katikati ya sebule kuna meza na viti. Ni asubuhi kama saa tano hivi Natala anapokuwa akipiga nguo za watoto pasi akiwa mchangamfu kwa kuchezachezesha mwili wake. Punde tu Gane anaingia na kuchezeana na Natala kuonyesha ujirani mwema wa wanawake hao. Kisha Gane anawaalika watoto wa Natala katika sherehe ndogo ya watoto wake na anaendelea kuueleza kuwa

alitumwa :(uk 2)

Natala: na nani?

Gane: chifu?

Natala: [*akikunja uso*] chifu?

Gane: mwenyewe amesema atakupitia baadaye leo.

Natala: (*akiweka pasi juu ya kikombe*) sikuelewi, gane.

Gane: [*kimzaha*] ni bora unielewe! Baadaye leo!

Natala: kuhusu nini?

Gane: nitajuaje siri ya watu wazima?

Mandhari haya yanambagua Natala kwa vile Gane anamdhania kuwa kwa vile bwanake anaishi mbali, wanaweza kuwa na uhusiano wa siri na chifu. Tila naye anaingia kuomba chumvi. Anapopewa anasema ni kidogo na alistahili kupewa nyingi. Wanabishana kidogo na Natala amtaka atoke kwa nyumba yake. Tila amwambia kuwa hawezi kutoka kwa vile alikuwa kwa nyumba ya kaka ya mumewe.

Mandhari haya yanatuonyesha jinsi wanawake wanawaonea wivu wanawake wenzao kuwa wao wana maisha mema kuwaliko hivyo wanastahili kuwapatia chochote kulingana na mahitaji yao. Pia habari ya "kifo" cha Tango Mwina inaletwa na Chifu ambaye hataki kumweleza Natala ambaye ni mkewe, bali anamtafuta Mzee Balu kwa vile wanaamini kuwa mwanamke hawezi kustahimili habari mbaya kama ya kifo, hasa kifo cha mumewe. Onyesho la pili laonyesha Wakene akiingia sebuleni mwa Natala na kuchukua picha ya Natala na kuanza kuikagua kwa makini huku akitabasamu. Kisha anaanza kuimba akichezesha mwili wake kuwa! (uk 11)

> "waniua ua kipenzi waniua ua
>
> waniua ua natala waniua ua
>
> waniua ua mrembo waniu ua
>
> waniua ua bure bilashi waniua ua"

Gane anamueleza Wakene kuwa hafai kusherehekea kifo cha nduguye kwani anayo nafasi sasa ya kumrithi Natala. Mandhari haya yanambagua mwanamke kuwa ni wazi kwamba ikiwa mumewe amekufa, ndugu yake ndiye anamrithi kama mkewe.

Bala mhudumu wa ufuoni anaendeleza ubabedume anapomwita Natala kama: "mwanamke unataka nini?" (uk 17) Hii ina maana kuwa Natala ni mwingine wala si kama wao.

Anaendelea kuambia maiti isilale kama mwanamke ambaye hulala kama gogo la mgomba. Bala anatumia maneno ya matusi ili Natala ajione kama mjinga na akubali ombi lake. Badala yake Natala amuambia kwamba hayo ayadaiyo ni matusi na mwanamke si mjinga bali ni binadamu kamili. Mandhari haya yanausawiri ushindi wa mwanamke katika juhudi za kujikomboa kutoka dunia hii ya wanaume. Kati ya yote Bala anayotaka kwa Natala yanamsawiri mwanamke kama asemavyo:

Ruth (1998:157) kuwa: kati ya majukumu ya mwanamke ni kuhudumiwa, kuunga mkono na kufurahisha wanaume.

Bala tena anamrukia akimtaka mapenzi lakini Natala amkabili na kumwangusha chini. Huu ni ushindi wa wanawake.

Onyesho la nne laonyesha ni wakati wa alasiri sebuleni mwa Natala na Tango Mwina. Natala amejifunga leso kiunoni na sehemu ya juu amevaa'T.Shirt', anajishughulisha na kupara karoti maganda, kisha Mama Lime abisha mlango.(uk 34) Katika mazungumzo yao Mama Lime amshawishi Natala abakie katika familia ya kina Tango. Anaendelea kusema kuwa katika mambo hayo ataongozwa na mila kwa sababu hayo ni matarajio ya ukoo. Anamweleza Natala kuwa furaha ya mke ni makazi, kula na kushiba, kuvaa nguo na kupata watoto, na kwamba zaidi ya mke mmoja ina manufaaa mengi. Mandhari haya

yanamsawiri mwanamke kama mtu ambaye anaongozwa na mila na ni sharti atii na kuenda na matakwa ya ukoo. Pia yanamsawiri mwanamke kama ambaye wakiolewa wengi na bwana mmoja ina manufaa mengi.

Katika onyesho la tano, ni asubuhi katika ofisi ya chifu. Afisi ina milango miwili.Chifu ameketi kitini akiangalia darini kama mtu aliyepotea katika mawazo yake mwenyewe.

Mlango mmoja unabishwa mara mbili bila chifu kusikia. Punde mlango unafunguliwa na Natala kuingia. Bwana Chifu anamfokea Natala kuwa ameingia bila kubisha. Anapouliza Natala swali akinyamaza, hivyo Amedharau serikali. Maswali yenyewe si ya serikali bali yanahusu mambo ya kinyumbani.(uk43) Mandhari haya yanambagua mwanamke. Maadam Natala ni mwanamke, yeye ni kuitika kwa yote ya mwanamume. Chifu anamwambia Natala kuwa yeye ni mrembo na kuwa atatafuta siku moja wakae mahali patulivu wanywe chai na soda huku wakipiga gumzo. Baadaye waelekee kwenda kucheza mziki kidogo. Anamwambia kuwa anajua mahali wakiporomosha zilizopendwa Utadhani unaelea juu angani. Chifu hapo anamtaka mapenzi. Anafikiria kuwa mwanamke yeyote ukimwambia maneno matamumatamu atakubali ombi la mume mara moja. Natala anapokataa ombi la chifu, chifu anakataa kumhudumia. Mandhari haya yanambagua mwanamke kuwa lazima amuhudumie mwanamume kimapenzi ndiposa aweze kupata huduma kutoka kwa mwanamume.

Onyesho la sita nalo ni kama saa nne na nusu asubuhi. Wakene ameketi kitini akipaka viatu rangi. Natala na Mzee Balu wanaingia uani.(uk 52) Wakene anamkabithi Mzee

Balu kiti na kumuacha. Natala na kusingizia kuwa hamuoni. Haya mandhari yanambagua Natala kwa sababu amekataa kumkubali Wakene awe mume wake. Hivyo hamuoni kama mtu. Baadaye anapoitishwa kutoa cheti cha shamba alichokichukua kutoka kwa Natala anashusha ugomvi akimfokea Natala kuwa hana haya kusema kuwa shamba la marehemu mumewe ni mali yake. Baada ya ubishi kwa muda Wakene anatoka nyumbani huku amebana bahasha kubwa kwapani akielekea kwa chifu. Wanamenyana hapo hadi anachukua cheti na Natala kumnyunyuzia Wakene maji ya pilipili.

Mandhari haya yanaonyesha jinsi mwanamke anavyotia juhudi kupigania haki yake. Chifu ambaye ana mamlaka na Wakene wana mipango ya kumpokonya Natala shamba lake lakini kwa juhudi zake Natala anafaulu kuchukua kile cheti. Mandhari yanaonyesha ushindi wa mwanamke katika harakati za kujikomboa kutoka mikononi mwa wanaume. Onyesho la saba laonyesha uani kwa Natala. Natala ameketi kitini akipara ndizi. Karibu naye chini , kuna ungo wenye mlenda ambao haujakatwakatwa. Sauti ya mwanamke akiimba kwa sauti ya chini inasikika.Punde, Mama Lime anatokezea. (uk 59) Mandhari yanaonyesha mwanamke anayewajibika kwa watoto wake na hata kwa wageni wanaomtembelea. Wazee wanamtuma Mama Lime kumwarifu Natala kukata ugwe wa wau unaodhuru walio hai. Natala alipokataa alimweleza kuwa ukoo mzima huwezi kuteseka kwa sababu ya ukaidi wa mtu mmoja. Wazee wanajua kuwa mwanamume akifa mwanamke sharti atekeleze matakwa ya jamii. Kwani asipofanya hivyo ataidhuru jamii nzima.

Mandhari haya yanambagua mwanamke kwa sababu hawampi mwanamke nafasi ya kuamua Maisha yake mwenyewe. Onyesho la nane pia lina mandhari uani kwa Natala na watoto wanacheza mpira. Mtoto mmoja analenga mtoto mwingine mpira, kisha kunasikika mgoto kwenye mlango ambapo Tila anaingia.(uk 63) Tila ameambiwa na watu kuwa Natala na Mama Lime wana mradi mkubwa wa thamana kama ya dhahabu. Mradi wa kuona kuwa Natala amechangiwa mume na Tila. Kwa kuwa Natala amefiwa na mume, kuwa Natala amemwahidi Mama Lime pesa ili amshawishi mumewe Tila(Wakene) amkubali Natala kama mke. Mandhari yanambagua mwanamke, ikiwa amefiwa na mumewe sasa amebaki akitapatapa waume wa wenyewe. La sivyo.Wanawake hawarithiwi kama kifaa. Tena watu wanawachochea wanawake ili watende matende yasiyo. Hata ingawa wazee wanataka mwanamke aridhiwe, lakini bibi ya yule mtu hatataka kuongezewa. Mwanamke akiwa peke yake yuatosheka. Mandhari yanatufunulia masengenyo wanakuwa nayo wanawake wenyewe kwa wenyewe wakati mwenzao amefiwa na mumewe.

## 5.2 WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA*

### 5.2.1 TANGO MWINA

Tango Mwina ni mumewe Natala na babake Alika na Bwanu. Yeye ni nduguye Wekene na shemejiye Tila. Ni mwanawe Mzee Balu. Tango anafanya kazi mjini na ni mwanamume aliyedhaniwa kuwa amekufa. Akadhaniwa kuwa ameletwa akazikwa kumbe ni mwizi aliyemwibia nguo na kitambulisho chake. Tango ni mwanamume ambaye ana mikosi mbaya sana. Hii inathibitishwa na kule kuibiwa nguo zake na

kitambulisho. Wakati mmoja askari walikua wanafanya msako, akaitishwa hongo shilingi hamsini ambazo hakuwa nazo.

Yeye na wengine ambao hawakuwa nazo walibandikwa kosa la kulewa na kuzururu wakiwa na nia ya kufanya maovu. Alishikwa na kutiwa kwenye seli na baada ya siku mbili walipelekwa mahakamani. Tango Mwina na wengine walikataa mashtaka hali ambayo iliwapeleka rumande mahali ambapo walikaa kwa siku kadhaa na kuteseka bila kuwasiliana na watu wa jamaa zao. Mwizi aliyekuwa amemwibia kitambulishona nguo alikufa, na kwa vile alikuwa na kitambulisho cha Tango, kukadhaniwa kuwa ni Tango Mwina ndiye aliyekufa.

Mkewe alisumbuliwa katika jengo la ufuo na katika kugharamia mwili ambao ulikuwa wa mwizi. Wanajamii nao wanamtaka arithiwe na Wakene ndugu yake Tango pamoja na watoto na mali yake Tango Mwina yote.

Tango ni mwanamume ambaye anawajibika kwa familia yake. Yeye anawaarifu kuwa angefika nyumbani baada ya siku saba. Tango anaporejea nyumbani baada ya kudhaniwa kuwa amekufa anachutama na kuwapokea kina Alika na Bwanu (watoto wake) aidha anawaletea vinyago, vibofu na vitabu vya picha. Anamshawishi Natala kuwa ni yeye mumewe aliyempenda. Anaporejea anamwokoa Natala kutoka taabu nyingi sana ambazo alizipitia wakati mumewe alipodhania kufa. Taabu hizo ni kama kurithiwa na Wakene, shamba lake pamoja na watoto. Anamwokoa Natala pia kutoka ujane, upweke, ugomvi, wivu na chuki kutoka kwa wanajamii kama vile Tila, Wakene, mwanamke fulani na

kadhalika. Anawaokoa wanawe kutoka uyatima na dhana kwamba hawatasoma. Tango si kama wanaume wengine kwa vile anawajibika katika kuendeleza maudhui ya mapenzi kwa familia yake.

### 5.2.2 NATALA

Natala ndiye mhusika mkuu katika tamthilia ya *Natala*. Ni mwanamke wa umri wa makamo hivi. Ni mkewe Tango Mwina na mamake Alika na Bwanu. Ni mkazamwana wa mzee Balu na shemejiye Wakene. Natala ni mwanamke ambaye amepigania haki za wanawake kwa jino na ukucha. Natala anakataa mila za kurithiwa kwa wanawake ambalo lilikuwa pendekezo la wanakijiji baada ya mumewe kudhaniwa kufa. Wakene ambaye ni shemejiye ataka kumrithi pamoja na mali na watoto wote. Hivyo anachukua cheti cha shamba na kupanga na chifu amuuzie shamba la nduguye marehemu. Natala anakabiliana naye na kumshinda kwa kumnyanganya cheti cha shamba. Pia anaonyesha ujasiri wake wakati anapopambana na mtunza jengo la ufuo aliyetaka hongo na mapenzi ya lazima, chifu naye na askari wote aliwashinda.

Natala ni mwanamke mwenye urembo wa akili. Hii inathibitishwa wakati anakashifu kitendo cha mtunza ufuo kurithi mke wa nduguye anayesemwa alifariki kutokana na ugonjwa wa kukohoa, kukonda na kutokwa vidonda. Huyu ni mwanamke aliye na mapenzi makuu kwa watoto na mumewe kwani wanawe wanapomwelezea kuwa mwanamke mmoja aliwambia kuwa hawatasoma anasikitika sana na kuwapa wote matumani ya kusoma. Natala anaonekana akiwatayarishia wanawe chakula na kuwasomesha vizuri. Mumewe anapotuma barua kuwa atarudi nyumbani baada ya siku

saba, Natala anafurahi na kuchezesha mwili wake huku akihesabu siku kwa vidole. Pia mumewe anapodhaniwa kufariki anakataa kufanya mapenzi na mlinda ufuo, chifu na kurithiwa na Wakene. Hii ni kuonyesha kuwajibika kwa mwanamke kwa familia yake. Natala ni kielelezo kwa wanawake ambao wamewajibika na kuwa na mapenzi kwa watu wa familia yake.

### 5.2.3 WAKENE

Mwanamume wa makamo ambaye ni mwanaye Mzee Balu na nduguye Tango Mwina. Ni shemejiye Natala. Wakene ni mwanamume anayetumiwa na wanakijiji kuendeleza utamaduni wa kumgandamiza mwanamke. Yeye na wanakijiji wanamtaka amrithi Natala kusingizia kuwa, ikiwa Tango mumewe amekufa, hataweza kujikimu na watoto. Wakati Natala anapokataa kurithiwa na Wakene, Wakene anaenda kwa Tango na kuchukua cheti cha shamba bila idhini ya Natala. Natala anapopigana na kumnyanganya cheti anamuita Natala "mwanamke."Hii inaonyesha kuwa anamdharau mwanamke kama mtu mwingine ambaye si sawa na wanaume. Tena mwanamke hastahili kung'ang'ana na mwanamume katika jambo lolote lile.

Wakene ni mwanamume mlevi asiyewajibika katika familia yake. Mkewe anaonekana akiombaomba chumvi, sukari, na mafuta taa kwa Natala, na asiyerithika na kiwango anachopewa. Katika ulevi wake anamwimbia mkewe ndugu yake wimbo wa mapenzi "waniua ua" wakati ana msiba. Hii inaonyesha kuwa ni mtu mwenye tamaa ambaye harithiki na vya kwake.Anachukulia kuwa, mwanamke anatumiwa kama chombo cha kumfurahisha mwanamume yeyote. Wakene ni mtovu wa adabu, ambaye anajibizana na

babake hasa pale kwenye mazishi ya Tango. Mzee Balu anapomwunga Natala mkono kwamba jeneza lisifunguliwe, Wakene anamwambia babake kuwa atakoma. Huyu ni mhusika kielelezo ambaye anaendeleza utamaduni. Ana taasubi ya kiume na ambaye anatumiwa na wanakijiji kuiendeleza ubabedume.

### 5.2.4 MTUNZA JENGO LA UFUO

Huyu ni mhusika ambaye uhusika wake umetokea kupitia mbinu ya mchezo mchezoni. Sehemu yake imetokea kama kisengerenyuma kuelezea kilichokuwa kimetokea nyuma. Sehemu yake imeigizwa na Bala kuzuia msomaji kujua sehemu au wajibu Bala alioutekeleza kibinafsi pale ufuoni alipoandamana na Natala kwenda kuchukua "mwili wa Tango". Ni mhusika ambaye ana taasubi za kiume na zinazothibitishwa kwa njia nyingi. Ili amtolee maiti, anaitisha hongo kutoka kwa Natala. Tena anamrukia kumlazimisha kimapenzi. Bala anamtusi maiti kuwa,"usilale kama mwanamke ambaye hulala kama gogo la mgomba." Anamrithi mke wa ndugu yake aliyefariki na ugonjwa wa kukohoa, kukonda na kuwa na vidonda mwili mzima. Mhusika huyu anaendeleza maudhui ya ufisadi, umaskini, taasubi ya kiume. Anatubainishia sifa za baadhi ya wahusika kama vile Natala kama jasiri na mwadilifu. Huyu mhusika ni kielelezo cha kiongozi mbaya asiyefaa kuigwa na ambaye anaendeleza ugandamizaji wa mwanamke. Mhudumu wa ufuoni anaendeleza ubabedume anapomwita Natala kama;"mwanamke unataka nini?"(uk47). Anatumia maneno ya kumdunisha mwanamke kama pale anampatia Natala kipande cha ndazi alichokuwa akila ili kumjaribu. Alipoona Natala akishika pua anasema kuwa amemtusi kwani alijua kuwa aliziba mapua ili asihisi harufu ya ufuoni. Yeye ndiye huhifadhi miili ya wafu.

### 5.2.5 MAMA LIME NA TILA

Hawa ni wanawake ambao wameathirika na utamaduni wa ubabedume. Hawampendi Natala ambaye anaonekana kuasi utamaduni wa ubabedume. Mama Lime anamshawishi Natala kwamba ni vyema abakie katika familia ya mumewe kwa kurithiwa na Wakene mumewe Tila. Tila ni mwenye maringo ambaye hataki kuitwa mwombaji wakati Natala anamkumbusha kuwa alimwomba sukari, mafuta taa, na sasa anaomba chumvi. Anapofika kwa Natala na kupata watoto wanakunywa uji anashangaa kwa kusema kuwa: "kumbe wanakunywa uji asubuhi!" Tila ni mwanamke anayependa ugomvi kama vile akishaomba chumvi kwa Natala anazidisha ugomvi kuwa (*anaiga jibu la Natala*) unataka nitumie neno gani na kuzidi kusema kuwa huchoki kuimba wimbo mmoja mwaka mzima! –"mafuta taa – sukari - ." Anamwendea Natala mbio anaposikia kuwa anarithiwa na Wakene mumewe. Mama Lime naye anaaminika na wazee kwa kupewa ujumbe ampelekee Natala kuhusu mila na desturi za ukoo. Ni mama ambaye anajua kudadisi sana. Alimuuliza Natala hali yake itakavyokuwa hasa baada ya muhimili kukatwa. Hapa alitaka kujua kama Natala amefikiria kutafuta mwanamume mwingine wa kumlinda baada ya mumewe Tango kufariki. Pia anamdadisi Wakene kile atakavyofanyia utajiri baada ya kuwa mbunge. Alijaribu kumshawishi Natala kuhusu umuhimu wa kurithiwa au kuwa mke wa pili. Natala anapokataa katakata ndio anaonyesha chuki kwa kusema kuwa "Nasema mara ngapi tulioa kwa watu wenye dharau na Natala ameurithi ujeuri huo kutoka kwao." Anadai kuwa shangaziye Natala anajifanya mgonjwa ili asihudhurie mazishi ya mwanetu. Analaumu Natala kwa jeneza kutofunguliwa. Tila na Mama Lime wanabainisha sifa za wahusika fulani kama vile Natala anayeonekana mwenye msimamo thabiti na mvumilivu.

### 5.2.6 GANE

Ni nduguye Tango na rafiki yake Natala. Ni mwanamke ambaye anawajibika kwa wanawe na wana wa jirani kama watoto wa Natala. Natala alipoenda ufuoni kuchukua "mwili" wa mumewe, Gane alishughulikia watoto wake. Pia alipotumwa na chifu kwa Natala kuwa alitaka kumuona, alifikisha ujumbe. Ni mcheshi hasa kwa Natala rafikiye. Hii inathibitishwa pale anapoingia kwa Natala na kumpata akipiga pasi na kusema "wanaopiga pasi tuingie "sisi sisi" "labda atakuja mzungumzie hilo jina na sura," "nitajuaje siri ya watu wazima." (Uk 1) Ni mhusika anayejenga maudhui ya ujamaa kwa kuwatunza watoto wake na wa Natala. Anawaalika tena watoto wa Natala na wa Amina kuhudhuria sherehe ya wanawe. Pia anachangia maudhui ya haki za watoto. Tena Gane anamnusuru Natala kwa kumtetea dhidi ya uvamizi wa kina Wakene waliotaka kumnyang'anya shamba, mali na watoto.

## 5.3 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA*

Mwandishi wa tamthilia ya *Natala* ametumia kiwango kizuri cha matumizi mbalimbali ya lugha kama ifuatayo: tashihisi, mani ya methali, mchezo ndani ya mchezo, jazanda, istiari, kinaya na nyingine nyingi.

### 5.3.1 TASHIHISI

Hii ni mbinu ya uandishi ambapo vitu visivyokuwa na uhai kupewa sifa za kuwa na uhai.Katika tamthilia ya *Natala* mbinu hii imetumika mahali kama :( uk7): "afadhali aje pekee. Singependa aje na mwenzake- pombe" (Uk16): "gari tulilosafiria halikuwa katika hali nzuri. Lilikataa kuwaka zaidi ya mara tatu. Kila lililogoma ilitubidi kulishawishi

kwa muda mrefu". Maneno haya yalisemwa na Bala nyumbani kwa Natala baada ya kurejea nyumbani kutoka ufuoni wakielezea matatizo yaliyowakumba njiani.

Uk16: Bala anapoigiza matendo ya mlinda ufuo akisema "nyinyi maiti niacheni nafasi! Hapa si nyumbani kwenu mlikokuwa mkikaa mtakavyo!... nini wewe! Usikodoe macho hapa! Huu si mchezo wa kuigiza...mlipopanda gari lililokuwa limejaa kupindukia mlikuwa mkifikiria nini? Mlijiona werevu sio... "Bado kuna nafasi tuingieni," sasa mmefahamu kuna gari la kusafiria na kwenye kaburi."

Uk21: "Gharama za maisha nazo ndizo hizo! Zimeota mabawa na kupaa angani".(Uk31): "Vyema! Nadhani tunaweza kuelewana bila safari ndefu ya maneno".(Uk42): "Tila hatachangia mume kwa mwanamke mwingine".

### 5.3.2 METHALI

UK3:"Palipo na moshi hapakosi moto." Gane anatumia methali hii kubainishia Natala kuwa kitendo cha chifu kutaka kumuona Natala ni dalili ya jambo fulani la siri labda kuanzisha uhusiano wa kimapenzi naye. (uk.15): "Hauchi hauchi unakucha". Natala walikuwa wamechelewa kurudi na, "mwili" wa mumewe kutoka ufuoni ambao sasa mlio wa gari unasikika, kuonyesha kuwa mwishowe wamefika.

(Uk 16): Bala akiigiza katika mchezo mchezoni akizungumza na maiti kuwa: "asiyefunzwa na mamake hufunzwa na ulimwengu," (Uk 21):

Bala: "Palipo na nia pana njia." Methali hii imetumika na mtunza ufuo akiigizwa na Bala wakati anataka waelewane na Natala ili Natala amhonge ndiposa amtolee maiti ya mumewe. (Uk31): 'Mti huenda kwa nyenzo.'Huyu ni chifu anayemshawishi Natala ili aweze kumhonga ndio akubali mazishi yaendelee. Methali na lugha iliyotumika inamdhalalisha mwanamke. Kila mhusika anamdhania Natala kuwa atashawishika baada ya kumshawishi kwa maneno machafu kama ya mlinda ufuo.

### 5.3.3 MCHEZO NDANI YA MCHEZO

Huu ni uigizaji unaofanywa na wahusika kwa njia ya kusisitiza kutendo cha awali.

Uk7: (*Akiigiza kulia*). Maskini Natala nimetoa siri zangu (*akijifanya kama kwamba anafuta machozi*) Hapa ni wakati Natala alipogundua kuwa Gane aliingia chumbani bila yeye kufahamu na akaweza kusikia yale yote aliyokuwa akiyafurahia. Kwamba imebaki wiki moja halafu labda Tango aje. (Uk 7): Sijui au niliongea na pipa la pombe (*anatembea na kuigiza sauti kutembea na uzungumzaji wa kilevi wa Wakene. Anaendelea hatua mbili mbele na hatua mbili nyuma huku ameinua mkono wa kulia* ) "msa – limiee Nata – la. Mwambi…e mwa – mbie nita – ku –ja kum – tembelea kesho. Kuna jambo ninge – pe – penda tuzungu– mze kesho.

Uk (16 – 22): Bala na Natala wanaporejea nyumbani kutoka ufuoni walipokuwa wameenda kuchukua maiti ya "Tango." Wanaigiza mateso aliyoyapitia Natala kutoka kwa mtunza ufuo. Bala anaigiza sehemu ya mtunza ufuo na Natala sehemu yake. Tila anabadilisha sauti na kuiga sauti ya Natala akimsihi Mama Lime azungumze na wazee

*Uk65: Waeleze ningependa kuendelea kuwa katika familia* ya marehemu mume wangu. Waeleze ningependa kuolewa na nduguye marehemu. Ukisha waeleza, ongea naye Wakene … bila yeye maisha yangu yatakuwa kama chakula bila chumvi.

### 5.3.4 JAZANDA

Hii ni mbinu ya utumiaji wa maneno yenye maana fiche ambapo maana zaidi inaweza kuzuliwa. Katika tamthilia ya *Natala* jazanda imetumika mara nyingi lakini tutaangalia baadhi yao tu.

Uk4: 'Huchoki kuimba wimbo mmoja mwaka mzima! Sukari, mafuta ya taa, Sukari, mafuta ya taa'… Haya ni maneno ya Tila akirudia maneno ya Natala kuwa ningekuwa mchoyo singekupa chumvi leo, sukari juzi wala mafuta taa siku nne zilizopita. (Uk 12): 'Mtambo! Ungepata fursa ya kujua kwamba Wakene ni mtambo wa umeme.' Maana fiche hapa ni kuwa Wakene ni mwanamume kamili.

Uk12: 'Ni ajabu kuona mboga ikijigamba katika mambo kama hayo'. Hii ina maana kuwa ni mtu ovyo asiye na uwezo.

(Uk23): 'Maskini watoto wangu hawajui kuwa kutoka sasa hawatakuwa na mikono miwili ya kuwahimili. Umebakia mkono mmoja tu.' Natala alimaanisha kusema kuwa kutokana na 'kifo' cha mumewe Tango, sasa ulezi wa watoto umebakia mikononi mwake pekee.

Uk35: 'Je! Umefikiria umuhimu wa kutafuta mhimili mwingine?' Haya ni maneno ya Mama Lime kwa Natala kutaka kujua kama amefikiria kutafuta mume mwingine baada ya 'kifo' cha Tango mumewe. 'Natala wataka ujue kuwa Wakene hayumo mikononi mwa mwanagenzi. Yumo kwenye viganja vya mganga stadi.' Hii ina maana kuwa Tila

anamtosheleza Wakene hivyo haitaji nyongeza ya utulivu wa mwili. Mama Lime naye anataka kujua kama ametafuta mume mwingine wa kumrithi kwa vile Tango ametoka na Natala alikuwa amezoea kukaa na mume.

*Uk 65 : 'Naona leo nimo mahakamani, na mahakamani kwenyewe nimekumbana na* wakili stadi kabisa. Ametafuna na kumeza vitabu vyote juu ya utaratibu wa kuhoji.' Hapa ni pale Tila amefika kwake Natala kuuliza kuhusu shaka zake ambapo anadhania Natala kuwa alitaka arithiwe na Wakene. Jinsi Tila anavyouliza maswali yake kijazanda ambapo Natala haelewi kwa haraka anamaanisha nini ndio sababu anamwita wakili.

**5.3.5 ISTIARI**

Hii ni mbinu ya uandishi ambapo mambo au vitu viwili hulinganishwa moja kwa moja. Pia mbinu hii imetumika katika tamthilia ya *Natala* kwa wingi kama vile:

(Uk 4): "Kwani wewe ni mungu? Unanipa chumvi kijiko kimoja kwani mimi ni mdudu?" Haya ni majibizano kati ya Tila na Natala wakati Tila alienda kuomba chumvi kwa Natala.

(Uk 5): 'Kwani unanifukuza? Kwani mimi ni mnyama wa mwituni?'

**5.3.6 KINAYA**

Mbinu hii ya uandishi huruhusu mambo kutendeka kinyume na yanavyotarajiwa. Mambo hayo ni kama: Tango anapodaiwa 'kufa,' mkewe anagharamia shughuli zote za mazishi. Anayapitia magumu kuanzia usumbufu alioupata pale ufuoni kutoka kwa mtunza ufuo.Baada ya mazishi nduguye Tango (*ambaye ni Wakene*) anataka kumrithi Natala pamoja na mali yake yote na watoto. Tango anaporejea nyumbani anamkuta

nduguye aking'ang'ana na mkewe akimnyanganya cheti cha shamba. Wakene ajidai kuwa yeye ni "*Wakene Bank International*" kuonyesha kuwa yeye ni tajiri ilhali anaomba usaidizi kutoka kwa Gane akiwa nyumbani kwa Natala. Bibi yake Tila naye anaomba sukari, mafuta ya taa na chumvi kutoka kwa Natala.

Uamuzi wa wazee kuwa Natala arithiwe na Wakene ni kinaya. Mama Lime anasema kuwa Natala alihitaji mhimili na muhimili mwenyewe ni mlevi na asiyewajibika katika familia yake. Wimbo anaoimba Wakene nyumbani kwa Natala unashangaza kwa sababu ni wimbo kuhusu mapenzi lakini anapoulizwa na Gane anadai kuwa anaomboleza. Wimbo wa mapenzi wakati wa matanga, ni kinaya hicho.Zile ndoto anazo Wakene kuwa anatarajia kuwa mbunge akishauza shamba ni kinaya. Anasema atajenga shule, hospitali, barabara, kuleta maji na kadhalika ambapo anafahamika yeye ni fukara na hawezi kufikia ndoto hii. Maneno ya Natala kwake Tila wakati alipokuja kumgombeza kuwa alitaka Wakene amrithi anasema: "Natala na Mama Lime wana mradi wa thamani kubwa kama ya dhahabu…na mradi wenyewe ni kuona kwamba Natala amechangiwa mume na Tila... Na ni kutoka sasa mpaka kaburi litakapowatenganisha." Hiki ni kinaya, kwa vile katika mazungumzo yao anaendelea kusema kuwa: "mimi, mimi Natala, nitake kurithiwa kama kifaa?... hata ningalikuwa nataka kuolewa upya, hata mumeo hangekuwa ameoa, hangeangukiwa na jicho la Natala! La! La Tila." Katika tamthilia chifu amechorwa kama mlevi, na mwenye kuitisha hongo kutoka kwa wafiwa na hata kuamua jeneza lililokuwa nusu kaburi kutolewa. Chifu pia kudai kuwa wanazika bila kibali ilhali yeye ndiye aliyetoa kibali cha kuenda kuchukua mwili kutoka ufuoni. Chifu tena kutuma ujumbe

kuwa mazishi kusimamishwa kumsubiri aje kutoa ruhusu. Hiyo ni kinaya kwa vile chifu ni mtu wa serikali ambaye anastahiki kukashifu ufsadi huo anaouendeleza.

## 5.4 HITIMISHO

Katika sura hii ya tano utafiti huu umeshugulikia usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Natala*, ambapo tumechunguza mandhari, wahusika na matumizi ya lugha katika tamthilia hiyo kwa upana. Kazi hii imehakiki jinsi mtunzi wa tamthilia amewasawiri na kuwahusisha wahusika wa kike katika kazi yake. Katika tahakiki hii ni wazi kuwa katika tamthilia ya *Natala* (2011) mwanamke anachukuliwa kama chombo cha kumfurahisha mwanamume. Yeye hana chake hasa wakati amefiwa na mumewe, anarithiwa yeye, watoto, shamba na mali yake yote na familia ya marehemu. Kuwa yafaa mwanamke kutii yote ya mwanamume hasa akimtaka mapenzi, ndipo aweze kupata huduma hata ingawa huduma ni ya serikali. Kisha katika tamthilia hii *Natala (2011)* ametuhakikishia kuwa mwanamke akitia juhudi kupigania haki yake atashinda. Pia ameonyesha ushindi wa mwanamke katika harakati za kujikomboa kutoka mikononi mwa wanaume

# SURA YA SITA: MUHTASARI

## 6.0 TATHIMINI NA MAPENDEKEZO

### 6.1 UTANGULIZI

Sura hii ndio ya mwisho katika utafiti wetu ambapo tumetoa muhtasari wa kazi yote katika tamthilia za Kithaka wa Mberia (2011) *Natala* na Ari Katini Mwachofi (2011) *Mama ee* kisha tukatoa mapendekezo ya utafiti kwa wale watafiti na wahakiki wa tamthilia hizi mbili wa kesho.

### 6.2.1 USHINDI WA WAHUSIKA WANAWAKE KATIKA TAMTHILIA YA *NATALA*

*Natala* ni tamthilia ambayo imeandikwa na Kithaka wa Mberia ambayo imejikita katika ubabedume. Inaiangaza jamii ambayo haimthamini mwanamke kama binadamu mwenzake mume. Hii inadhibitishwa wakati Tango Mwina mumewe Natala alipokisiwa kufa, Chifu ambaye ndiye aliyeleta habari hiyo, hakutaka kumwambia Natala kwanza, kwa sababu alijua kuwa mwanamke hawezi kustahimili habari mbaya kama ya kifo hasa kifo cha mumewe. Kwa hivyo anamtafuta mzee Balu na kumwelezea juu ya "kifo" cha mwanawe. Wakene nduguye Tango anaonekana akiimba wimbo wa furaha wakati habari ya kifo cha nduguye imewafikia. Gane anamwelezea kuwa haifai kusherehekea kwani sasa alikuwa na nafasi nzuri ya kumrithi Natala.

Bala mhudumu wa jengo la ufuo anaendeleza ubabedume anapomwita Natala kuwa "Mwanamke! Unataka nini?" (uk.17) anaendelea kutusi maiti kuwa yasilale kama mwanamke ambaye hulala kama gogo la mgomba. Maneno haya yote yalikuwa kumweka Natala kujihisi mnyonge na akubali ombi la mtunza ufuo kwa kutoa hongo na kujiachilia kimapenzi naye. Natala badala yake anamjibu kuwa yeye si mlango wa jengo la umma kuguswa na kila mtu, huku akijitenga. Kujikinga kutokana na shambulizi la Bala anamwambia kuwa hayo ayadaiyo ni matusi na mwanamke si mjinga bali ni binadamu kamili. Bala anapomrukia Natala, Natala anampokea na kumpitisha chini na kuanguka kwa magoti na mikono kutoa picha ya mnyama anayesimama kwa miguu minne. Anaposimama Natala anamsubiri kwa ukakamavu mwingi. Kwa vile Bala hana jibu la kumpa Natala, Bala anakimbilia dini kuwa mwanamke alitoka kwa mwanamume hivyo yeye si binadamu kamili bali kifupa tu cha mwanamume.

Katika jengo la ufuo tena kuna mahali Bala anamuomba Natala pesa ili aweze kumtolea huduma. Jibu la Natala lilikuwa: "wacha kunizungusha, unalipwa kila mwezi. Fanya kazi unayolipiwa." Kwa vile Bala alishindwa la kujibu, anatisha kuondoka bila kutoa huduma. Huu ni ushindi wa Natala katika kutetea haki yake.

Siku ya mazishi ya "Tango", Mama Lime, Tila na Wakene wanashirikiana kwamba lazima wauone mwili wa marehemu mwanao kabla hujazikwa, Natala anakataa katakata kwa kuwaeleza kuwa uso wa marehemu umepondekapondeka vibaya na asingetaka umuongezee majonzi wala kuwapa watoto wake jeraha la milele.

Kuhusu kurithiwa na Wakene,...mama Lime anamwambia Natala kuwa mambo hayo yataongozwa na mila ambayo ndiyo matarajio ya ukoo. Natala anapinga maneno ya Mama Lime kuwa; Hana haja ya kuacha nyumba waliyoijenga na mumewe na ataendelea kulima. Yeye aliendelea kuwa ataongozwa na fahamu zake na wala si mila katika kufanya maamuzi. Natala anasema kuwa anataka kuwalea watoto wake na wala hataki kurithiwa na Wakene ati kwa sababu mila inamtarajia kukubali. Yeye mwenyewe atayaendesha maisha yake na haamini kuwa nyumba ya zaidi ya mke mmoja ni faida kwa mwanamke asemavyo Mama Lime. (Uk.39-40).

Mama Lime ameathirika na ubabedume na anaamua kuondoka kwa vitisho anavyoviita ushauri ambapo anakimbia kuripoti kwa wanakijiji. Wakene, Mzee Palipali na Mama Lime kwa pamoja wanakuja kumshambulia Natala. Walikuja kumpokonya nyumba, watoto, shamba pamoja na fedha zilizokuwa kwenye benki, kusingizia kuwa ameketaa kurithiwa kama ilivyo desturi. Huu ni ubabedume ambao humchukulia mwanamke kuwa hastahili kumiliki kitu chochote hata watoto aliowazaa mwenyewe. Kama asemavyo:
Spivak (2004:479) kuwa katika kile kiitwacho jamii ya mama na baba, umiliki wa kisheria wa mtoto ni ukweli usiogeuka kuwa mtoto ni mali ya mwanamume anayemzalisha mwanamke. Mwanamume huhifadhi hati miliki juu ya zao la mwili wa mwanamke. Wakene anapojaribu kutoka na cheti cha shamba, Natala anapigana naye hadi anamnyanganya cheti. Wakene ajaribu kumcharaza Natala kwa mshipi, Natala naye atumia kikaango na mwiko kumcharaza badala yake. Mara zote Natala ajikinga kwa kikaango kisha alifaulu kumpiga Wakene teke kwenye suruali chini ya kitovu. Kutokana na uchungu mkali akiwa ameshikilia mshipi mkononi Wakene aanza kutembea kwa

mwendo wa mwenye maguru bata akielekea lango la ua. Natala anamsindikisha kw mapigo mara kichwaani kwa kikaango na wakati mwingine mgongoni au mabegani kw mwiko. Hapo ndipo wanapokutana na Tango akiwasili nyumbani na kuchukulia kuwa n mzuka wake. Huu unaonyesha ushindi wa Natala. Natala anafaulu kutetea imani n mtazamo wake katika maisha. Tango anapowasili watu wote wanatoroka wakidhani n mzuka. Natala anamwambia Tango kuwa "...sina kosa. Nilikuwa napigania haki yang na haki ya watoto wangu." Hii inathibitisha kuwa si lazima mwanamume awepo ndip mwanamke aweze kutenda jambo au kupigania haki yake. Tamthilia ya *Natal* inamsawiri mwanamke kama mshindi katika juhudi na harakati za kutafuta ukombozi w mwanamke. Natala amepambana na vizngiti katika juhudi zake za kumkombo mwanamke dhidi ya jamii hii ya ubabedume hatimaye anafaulu wakati anamyangany Wakene cheti cha shamba na kumchapa kwa kutumia kikaango hadi pale wanopkutana n Tango kwa mlango na kudhani kuwa ni mzuka.

### 6.2.2 USHINDI WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAMTHILIA YA MAMA EE.

Tamthilia ya Ari Katini Mwachofi (2011) *Mama ee* imegawika katika sehemu mbil Ugawaji huu umedhamiriwa kuonyesha mabadiliko ya msimamo wa nguli na wa mtunz Katika sehemu ya kwanza, wahusika wakuu wanajaribu kuishi kulingana na itikadi z kimapokeo zinazotokana na utamaduni, mfumo wa kuumeni na dini. Kaida ya itikac hizi ndizo zinazowafanya Mwavita na Tenge kushehenezwa na kustahimili aina zote z dhuluma.

Sehemu ya pili inawasawiri wahusika wakuu wenye ari na nia ya kujengua ulimweng

wa kimapokeo na kuufinyanga ulimwengu huo upya. Mwavita na Tenge amba

wamekua kimawazo kutokana na dhuluma walizozipitia katika sehemu ya kwanz

wanadhamiria kuwakomboa wanawake wenzao kwa kuwaelimisha. Na ikilazim

watazusha vita na fujo kama vyombo vya kufaulisha dhamira zao.

Mwachofi ametumia mbinu mbalimbali katika kuwasilisha ujumbe wake. Mbi

muhimu aliyotumia mtunzi ni uhuishaji wa sauti ya kike na uipaji sauti hiyo nafasi

kujieleza na kujisemea. Maoni na mawazo ya Mwavita yanahitilafiana na matamshi

hekima yanayotongolewa na wazee. Hekima inayobobea katika methali, mafumbo

mawaidha mengine yanayorekodiwa katika maandiko matakatifu kama Bibilia. Hii i

maana kuwa licha ya kurejelewa mara kwa mara haimbadilishi Kinaya wa

kuhurahisisha ugomvi kati ya Kinaya na Mwavita. Kutokana na maongezi kati

mahakama tunaonyeshwa wazi kwamba mahakama inawapendelea wanaume kuwamili

na kuwakandamiza wanawake.

Mbinu nyingine ni ya matumizi ya majina ya kimajazi ili kufafanulia nyadhifa

wahusika wakuu. Jina Mwavita linatokana na neno 'vita'. Mbinu hii inajidhihiris

wakati Mwavita anapigana vita dhidi ya maonevu ya kila aina: nyumbani kwake na ha

ulimwenguni kote. Vita vya Mwavita ni vita vya wanawake wote wanaonyanyaswa

wanaume. Jina Tenge nalo lina maana mbili, maana ya kwanza ni kuwa 'kombo'

maana ya pili ni 'fujo' au 'ghasia.' Maana hizi zinatuelekeza kuwa Tenge ni mwanam

mbaya. Haya pia yanajitokeza wakati Tenge alitungwa mimba kabla ya kuole

tunaweza kusema kuwa yeye ni kombo. Pia Tenge anawasababishia fujo watu wote wanaomdhulumu. Kinaya ni jina linalo maana ya kinyume. Ni mhusika muhimu kwa vile anakuwa kiwakilishi cha wanaume wengi ambao wanaamini kwamba mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume badala ya mwanamke kuwa msaidizi wa mwanamume.

Mbinu inayotumika kuwasilisha ujumbe kwa walimwengu wengine wasiokuwa jukwaani ni ritifaa. Katika tamthilia ya *Mama ee* imetangulizwa na ushairi. Ushairi huu unawahutubia wanawake na wanaume. Wanaume wanaonywa kwamba wanawake hawastahili maonevu tena. Kwa upande mwingine wanawake wanachochewa kujifungata mazombo na kujibwaga katika uwanja wa harakati za ukombozi. Mwavita ameshirikiana na Tenge dadake kupambana na asasi zote kama ndoa, dini, sheria, chama cha wanawake, elimu, utamaduni na mila, pamoja na mahakama au koti. Hatimaye wameshinda baada ya kumchapa Kinaya. Mwavita na Tenge wameanzisha chama cha wanawake ambacho kinawahusisha wanawake wote. Walio mjini na wa vijijini ili washirikiane pamoja kubadilisha jamii ambazo zina mielekeo ya kumkandamiza mwanamke. Katika tamthilia ya *Mama ee* Ari Katini Mwachofi amewasawiri na kuwajenga wahusika wa kike vizuri sana hasa Mwavita. Kwa vile Mwavita amekumbana na changamoto nyingi za kumkata moyo wa kuendelea kutia juhudi katika kumkomboa mwanamke, hatimaye alishinda.

### 6.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Kazi hii ya utafiti imeshughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kithaka wa Mberia *Natala (2011)* na Ari Katini Mwachofi *Mama ee (2011).* Utafiti huu

umechunguza jinsi wahusika wakuu katika kila tamthilia wanajaribu kupigania ukombozi wao kutoka kwa dunia hii ya wanaume. Utafiti zaidi waweza kufanywa kuhusu wahusika vijana au wahusika wakongwe katika tamthilia hizi mbili. Utafiti huu ulijikita zaidi katika nadharia ya ufeministi ambayo inapigania usawa mwiongoni mwa wanadamu na inaonyesha udhaifu wa mfumo dume. Inapigania uhuru wa mwanamke kwa kudai kuwa ana haki kupata na kufurahia haki zote za binadamu. Utafiti zaidi unaweza kutumia nadharia jingine katika kutafiti usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia hizi mbili.

# MAREJELEO


Aristotle (1965); *"Poetics" Katika S.T D, Aristotle/ Horace/ Longinus*. Harmondsworth: Penguin

Banks O. (1990); *Faces of Feminist*. Canbridge: Basil Backwell.

Cameron D.(1990); *Feminism critique of language.Feminisim*. A Reader, London Routeledge.

De Beauvoir S. (1972); *The Second Sex.* London: Pan Books Publishers.

De Lauretis T. (ed) (1986); *Feminist Studies/Critcal Studies*.Wisconsin: Macmillan Press.

Eagleton T. (1992); *Marxism and LiteraryCriticism*. London: Routledge.

Ellman M. (1968); *Thinking about Women*. New York: Harcout.

Forster, E.M ( 1927); *Aspects of the Novel*, London; Penguin Boots

Freidan B. (1963*); The Feminine Mystique*. NewYork: Dell.

Gill, R(1985); *Mastering English Literature London*; The Macmillan Press Ltd.

Greer G. (1981); *The Female Eunuch*. London: Grafton Books.

Holman (1936); *A Handbook to Literature,* Odyssey, New York.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004); Oxford University Press

Katola E. (2006*); Udhalimu dhidi ya Wahusika wa Kike*. Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kiango S. (1997); *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya*.Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kimani N na Wafula R.M. (2007*); Nadhria ya Uhakiki waFasihi* J.K.F. Nairobi.

Kithaka wa Mberia (1997); *Natala.*Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Kruger (1996*); Female Character in Contemporary Kenya's Women Writers*. Figures subdued Voices, Madson: University of Nairobi.

Lugano R. (1989); *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi.* Tasinifu ya M.A: Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mazrui A. (1981); *Kilio Cha Haki*. Nairobi: Longman.

Mbatiah M (2001); *Kamusi ya Fasihi*; Standard Textbooks, Graphics and Publishing.Nairobi.

Millet K. (1970); *Sexual Politics*. NewYork: Doubleday and Company.

Millet, K. (1969); *Sexual Politics London*: Virago.

Mlokozi M.M (1979); *Mukwava wa Uhehe*. East African Publishers Ltd: Nairobi.

Moers E. (2003); *Literary Women* .London:The Women's Press.

Mohammed S.A (2000); *Kitumbua Kimeingia Mchanga* Nairobi: Oxford University Press

Moi T. (2003); *Sexual/ Texual Politics* (2nd Ed). London: Routledge.

Momanyi C. (1998); U*sawiri wa Mwanamke Mwislamu katika Jamii ya Waswahili inayobainika Katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta: (Haijachapishwa.)

Morgan R. (1992); *The World of Women*. New York: Norton and Company.

Moteith M. (ed) (1986); *Women's Writing. A Challenge to the Theory*: New York: Harvester Press

Msokile M. (1993); *Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East African Educational Publishers Ltd. Nairobi.

Mugambi E. (1982); *Uhakiki Wa Maudhui Katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya Zilizochapishwa:* Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu Cha Nairobi .(Haijachapishwa)

Mulila J. (2007); *Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake*. Tasnifu ya M.A ya chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutua J. (2007); Mtazamo wa vijana na Wazee kuhusu Udhalimu wa Mwanamke katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingi Mchanga*: Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwachofi A.K. (2011); *Mama ee* : East African Publishers Nairobi.

Mweri J.G. (2010); *Utangulizi wa Isimu:* K.L.B, Nairobi.

Ndungo,C.M (1985) ;*Wanawake na Mabadiliko ya Kihstoria Katika Fasihi Ya Kiswahili ya M.A.* Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa)

Njogu na Chimerah (1999); *Ufundishi wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi Jomo-Kenyatta Foundation Ltd.

Nyaberi H. (1997); *Mwamko wa Wanawake katika tamthilia za Penina Muhando.* Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Nyaosi (2008); *Taswira* ya *Asasi katika Riwaya ya Kiu na Msimu ya Vipepeo.*

Ogundipe. M. (1994); *Recreating Ourselves*: African Women and Critical Transformation (Journal).

Osiemo D.O (1997); *Fani Katika Ushairi wa Mwalimu Mbega*, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ruth S. (1998); *Issues in Feminism-An IntroductionTo Women Studies*. Harmondworths: Penguin.

Sapir E (1921); Language, New York: Harcourt Brace

Showalter E. (1971); *Women's Liberation and Literature*. New York: Harcourt Brace. Jovanovich.

Steady (1981); *Reflecting on the Politics of Sisterhood*, African Word Press, New York.

Stitcher S.B and Parpart J.L (1998); *Patriachy and class-African Woman in the Home and the Workforce*. London: Westview Press.

Strobel M. (1979); *Muslim Women in Mombasa 1890- 1975*: New Harren and London. Yale University Press.

Strobel M.(1979); *Muslim Women in Mombasa (1890-1975)* and London.Yale University Press.

Sylvester C. (1995); *Feminist Theory and International Relation in a Postmodern Era.* Cambridge: Cambridge University Press.

Tuttle (1986); *The English Dictionary.*

Wafula R.M na Njogu K. (2007); *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Jomo Kenyatta Foundations Ltd, Nairobi.

Wamitila K.W. (2003); *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi Focus Publications Ltd, Nairobi.

................. (2002); *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele vyake*. Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

.................. (2003); *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi. Focus* Publication Ltd, Nairobi.

.................... (2008); *Kanzi ya Fasihi; Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide – Muwa Publishers Ltd, Nairobi Webster (1970); *The Saurus Dictionary Concise.*

Wepo Wasa (2005); *Fani katika Utenzi wa Siri Li Asirali na Utenzi wa Mwana Fatuma.*Tasnifu Ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wollstonecraft, Mary,(1972); *A Vindication of the Right of Woman.*Boston:PerterEdes.

Woof V. (1929); A *Room of Ones Own.London.* The Hugarch Press.